# Nipashe

Jumatano Julai 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581747

www.ippmedia.com **MWANGA WA JAMII**

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**Mama**, baba wafariki dunia wakisafirisha mwili wa mtoto

UKURASA 5

**Jela** miaka 180 kwa kupora simu, fedha, Tv kwa panga

UKURASA 5



**Mgombea** urais mwanamke USA azua kiwewe, kila jimbo lamkubali

UKURASA 19


siasa

JUMATANO JULAI 24, 2024 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

BEN MKAPA 1938-2020 Mpiganaji anayeishi akizidi kuonyesha njia kujenga uchumi bora na shindani

BENJAMINI MKAPA-1938/2020

Ni kiongozi shujaa ndani na nje asiyeweza kusahaulika

UKURASA 11

## RIPOTI MAALUM

# Mifuniko ya 'mamantilie' inavyokaribisha saratani

UKURASA 2



Mamalishe akiandaa chakula kwa ajili ya wateja wake, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Bundi wazua taharuki shuleni, wanaswa kwa njia maombezi

UK. 15



Waumini wa Kanisa TAG KFC Kiomboi (kutoka kushoto), Yohana Yohana, Josephat Mwendo na Elliah Mgina, wakishika bundi baada ya kuwatoa katika dari la moja ya madarasa ya Shule ya Msingi Igumo, wilayani Iramba mkoani Singida juzi, ambako wanafunzi wake walikumbwa na mapepo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

UKURASA WA 3

## VIGOGO WA TTCL, UCSAF, SHIRIKA LA POSTA WATENGULIWA



RAIS Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa viongozi wakuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)...

# Mahakama yasimuliwa mama, mwana walivyoua binti kikatili

• **Yadaiwa** walilenga asitoe ushahidi ...

*Endelea ukurasa 4*

**MICHEZO** **BALOZI: KWA SIMBA HII TIMU ZIJIPANGE** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Mifuniko ya 'mamantilie' inavyokaribisha saratani

**Na Beatrice Shayo**

MIFUKO ya plastiki imethibitika kisayansi ni hatari kwa mazingira na afya ya binadamu na viumbe wengine.

Serikali ya Tanzania ilishapiga marufuku kuzalisha, kusambaza, kuuza na kutumia mifuko hiyo tangu Juni Mosi, 2019.

Hata hivyo, baadhi ya wapishi na hasa mamalishe na babalishe, wakiwamo wa mkoani Dar es Salaam, wanaitumia kuhifadhi chakula na hivyo kuziweka hatarini afya za walaji.

Mwandishi wa Nipashe amebaini baadhi ya wafanyabiashara hao wa chakula hutumia mifuko hiyo ama kupikia chakula au kuhifadhi chakula kama nyenzo maalum ya kuwezesha kiendelee kuwa na joto.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa mifuko hiyo inapopata joto katika chakula, inazalisha chembechembe ambazo ndio wakala wa kusababisha saratani.

Ni ufafanuzi unaotolewa na wabobevu wa eneo hilo la tiba, wakioanisha uzoefu, ushuhuda na yaliyomo katika utafiti mbalimbali.

Sharifa Mohamed, mamalishe katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam, anasema hutumia mifuko ya plastiki kufunika chakula chake anapomaliza kupika, akiamini inasaidia kutunza joto.

"Nikifunika kama hivi nikija kupakua, chakula kinakuwa cha moto. Mfuko huu (anaushika) hauyeyuki wala hautoi chochote, ni kama unavyoona, haujalainika, chakula kina moto," anasema Sharifa.

Mamalishe huyo anasema hajui kama mifuko hiyo si salama kiafya, akisisitiza yeye pia hula chakula hichohicho anachoandaa kwa ajili ya wateja, hata kikibaki baada ya kufunga biashara, hupeleka nyumbani kuliwa na wanafamilia.

"Hii mifuko si kwamba inayeyuka katika chakula, inabaki hivihivi. Mifuko hii ninaipata kwa wauzaji sukari, ule mfuko wa ndani ya mfuko wa sukari ndio ninachukua kwa ajili ya kufunikia chakula," anasema Sharifa.

Mamalishe huyo anasema huifua mfuko wa aina hiyo huutumia kwa kipindi cha hadi miezi mitatu, akiifua baada ya kazi.

"Baada ya miezi mitatu unaanza kuona mfuko huu umechoka, unatafuta mwingine, unabadilisha.

"Nikimaliza kuuza chakula, changu ninakwenda kuufua huu mfuko, ninauanika, kesho ninaendelea kufunikia tena chakula. Inanisaidia sana kuhifadhi chakula kiwe na joto," anasema Sharifa.

Mjasiriamali anayeuza mihogo ya kukaanga Buguruni, jijini Dar es Saalam, Brigita Kristian, anashauri serikali iwezesha upatikanaji vifungashio mbadala ambavyo vitawasaidia katika kufanya biashara.

"Mtu anakuambia niwekee mihogo mitatu, kachumbari na pilipili, ina maana ukimwekea katika vifungashio vya bahasha, inachanika na matokeo yake mihogo inadondoka.

"Hata hii mifuko laini ambayo tunawawekea wateja, inaungua. Inanibidi niweke miwili ninapohudumia mteja na bado tunapata shida," analalama mjasiriamali huyo.

Brigita anasema hana uelewa kama mifuko hiyo inasababisha mtu kuugua maradhi ya saratani.

"Kitu mbadala cha kutumia labda wateja wajinunulie kontena, nina baadhi ya wateja wangu wa hapa karibu huwa ninawawekea katika sahani zangu.

"Sasa kwa hawa wapitanjia, hawana kontena, inatubidi tuwawekee katika mifuko ya plastiki.

"Bado tupo kwenye wakati mgumu, hata hii mifuko ambayo imezuiliwa wametupandishia bei, hivi sasa inauzwa Sh. 1,500 wamepandisha kwa sababu imepigwa marufuku na ile mifuko ya bluu ukiweka vitu vya moto, kunatokea shida ileile, inayeyuka," Brigita anasema.

Mjasiriamali huyo anasema elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi, wanapokwenda kununua chakula, wawe na chombo cha kubebea ili kuepuka vifungashio vya plastiki vyenye madhara kiafya.

Godfrey Minja, mfanyabiashara katika soko la Buguruni, anasema serikali inapopiga marufuku matumizi ya mifuko plastiki, iwezeshe upatikanaji vifungashio mbadala ambavyo ni rahisi kwao kuvipata na kuvitumia kulinda afya za walaji.

"Wamepiga marufuku mifuko ya plastiki lakini watu wanaendelea kuitumia. Je, mbadala wa hivi vifungashio ni upi ili tuache kuvitumia?

"Kuna kipindi tunaambia aina fulani ya mifuko ndio inatakiwa na serikali baada ya muda hawaitaki tena. Wanatuchanganya sisi wananchi, hatujui serikali inataka ipi.

"Hivyo viwanda vinavyozalisha huenda ni vyao wenyewe viongozi wetu huko serikalini, unaweza kukuta mwanasiasa ana kiwanda chake hatuwezi kujua.

"Hii mifuko ambayo imepigwa marufuku na serikali ndio inayozalisha fedha nyingi, inachafua mazingira lakini inazalisha fedha," mfanyabiashara huyo anadai.

**HATARI YA SARATANI**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam, Harrison Chuwa, anasema kuna uwezekano wa kupata saratani kutokana na matumizi ya mifuko ya plastiki katika kupika na kuhifadhi chakula.

Bingwa huyo anaeleza kuwa kwa Afrika, plastiki zinazozalishwa au kuingizwa barani, zikipata joto zinatoa vipande vidogo vya plastiki vyenye sumu.

"Mfano, kwa viumbe baharini wataalamu wamebaini samaki wakila plastiki, wanakufa au kuharibu mfumo wao wa chakula kutokana na hizo chembechembe za plastiki.

"Chembechembe hizo ni hatari kutokana na kuwa na kemikali ambazo zinatokana na plastiki zinapopata joto, kuna kemikali nyingi zinazotumika kutengeneza plastiki na kuzifanya ziwe laini.

"Plastiki ni kama PVS ambazo ukiziona zinakuwa ngumu, ili kuifanya iwe laini, wanatumia kemikali ambazo ni hatari zinapoingia katika mwili wa kiumbe hai," bingwa huyo anasema.

Dk. Chuwa anasema aina nyingine ya kimekali huifanya plastiki hata ikianguka isipukutike, na kwamba kwa wanyama kemikali hizo zimethibitika zinaweza kusababisha saratani.

"Kuna utafiti ambao ulifanywa India miaka miwili iliyopita, waliona kuna ongezeko la saratani ya koo na ugumba kwa sababu kule hata chai wanakunywa kwa kutumia kikombe cha plastiki. Watafiti walianglia kama matumizi hayo ya plastiki yanachangia ongezeko hilo la wagonjwa," anasema Dk. Chuwa.

Hata hivyo, bingwa huyo anasema kuwa mpaka sasa hakuna utafiti unaoonesha moja kwa moja kwamba plastiki zinasababisha shida hiyo, ingawa maabara za wanyama zimeonesha kemikali mbili zilizomo katika plastiki zinaweza kusababisha saratani.

Ofisa Afya wa Jiji la Dar es Salaam, Reginald Mlay, anasema huwa wanatoa elimu katika masoko na kuzungumza na mamalishe na babalishe kuhusu madhara ya matumizi ya mifuko ya plastiki katika kupika na kuhifadhi vyakula.

"Kubadili tabia za watu kunahitaji kuwa na muda wa kutosha kwenye suala zima la ubora na usalama wa chakula kinapoandaliwa hadi kumfikia mlaji, tuhakikishe kinafika katika hali ya usalama," anasema Mlay.



Mamalishe akiandaa ugali kwa ajili ya wateja wake katika eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JOHN BADI**

Ofisa Afya huyo anathibitisha kuwapo matumizi ya mifuko ya plastiki kuhifadhi na kupika chakula katika eneo lake la kazi. Anasema wanafanyia kazi changamoto hiyo kwa kutoa elimu.

Anasema kuwa mwaka 2021, kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), walitoa elimu kwa mamalishe katika maeneo yenye watu wengi jijini, akiyataja kuwa ni pamoja na Soko la Kimataifa la Samaki Feri, Ilala, Mnazi Mmoja, Karume, Buguruni, Tabata na Gongolamboto.

"Mifuko ya plastiki imethibitika kisayansi inatoa chembechembe ambazo zinapopata moto zinaweza kusababisha ugonjwa wa saratani baadaye.

"Watu wengi wanavyotumia hawaoni shida kwa sasa, kumbe ni tatizo linalojikusanya kidogokidogo, itafika wakati unaona fulani ana tatizo la saratani ya utumbo, utumbo mkubwa, kwenye midomo, mikono, mguu kutokana na tatizo hilo," anaonya Mlay.

Ofisa huyo anasema mamalishe na babalishe wanaweza kutumia vifungashio mbadala wa bahasha na foili katika kuhifadhi vyakula vya moto ili kulinda afya ya mlaji.

Anasema maeneo mengi wanatumia foili kufunga vyakula na upatikanaji wake kwa sasa ni gharama nafuu, hivyo wanaweza kutumia ili kulinda afya za wananchi.

Katazo la mifuko ya plastiki ni utekelezaji wa kifungu cha 230(2)(f) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Kwa mujibu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC, tani 350,000 za mifuko ya plastiki huzalishwa kila mwaka.

Hata hivyo, baraza hilo linabainisha kuwa chini ya asilimia 10 ya mifuko iliyotumika hurejereshwa, likiwa na angalizo pia kwamba mifuko ya plastiki huchukua miaka 400 mpaka 1,000 kuoza ardhini.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN) ya Mwaka 2018 kuhusu madhara ya mifuko hiyo, inaonesha viumbe wa majini wanaathiriwa na hata kufa kutokana na kuingia kwa bidhaa za plastiki baharini.

Meneja wa NEMC Kanda ya Temeke, Anord Mapinduzi, anaungana na wataalamu waliotangulia kwamba, wananchi wanaweza kupata magonjwa ya saratani kutokana na matumizi ya mifuko hiyo katika kupika au kuhifadhi chakula.

Anasema mifuko hiyo ina kemikali aina ya Bispheno 4 ambayo anaitaja ni hatari kwa afya za binadamu, hususani kwa wanaotumia mifuko hiyo katika kupika au kuhifadhi chakula ili kiendelee kuwa na moto.

HABARI KITAIFA

# Miili ya wanawake yakutwa imetupwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MIILI ya wanawake wawili imekutwa katika Mtaa wa Chinyika, Kata ya Mkonze jijini Dodoma, huku mmoja ukidaiwa kuwa na majeraha, ukiwa umefungwa katika mfuko wa plastiki, boksi na kiroba.

Kwa mujibu wa mashuhuda, mwili huo umeonekana ukiwa na majeraha yanayotoa ishara ya kudhuriwa kwa kitu chenye ncha kali.

Akizungumzia tukio hilo juzi, Mwenyekiti wa mtaa huo, Aloyce Maswikwi, alisema matukio hayo yalitokea katika mtaa wake kati ya juzi na jana. Mmoja kati ya wanawake hao hajatambulika.

"Inaonekana aliyemuua alikwenda kununua godoro, akatoa nailoni ya lile godoro, akamfunga na nguo, akamchomeka katika mfuko na kisha kumfunga na mpira.

"Pia alitafuta maboksi, akamlaza marehemu akamfunga na mipira hii ya bodaboda, mzigo umefungwa kweli kweli. Mimi na macho yangu ninaona," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa baada ya hapo, muuaji alichukua kiroba cha kuhifadhi mahindi cha madebe saba, akamweka na kisha kufunga na mpira.

Alisema mzee mmoja aliyetoka kuchunga mifugo yake, alikwenda katika korongo hilo kwa ajili ya kunywesha ng'ombe wake, aliona kitu kama mzigo wa mtumba ukiwa umetupwa katika eneo hilo.

"Akamwita mwenzake, 'njoo tuangalie, kuna mzigo gani?' Alipokwenda wakasema 'ngoja tufungue kuna nini', hali iliyowafanya kuchana, walipokuwa wamechana waliona miguu ya mtu," alisema.

Mwenyekiti huo alisema walichana mfuko kisha boksi, mfuko wa godoro na kukutana na nyayo za mtu, hali iliyowafanya kuruka kwa mshtuko kwa kukuta mtu badala ya mzigo wa mtumba kama walivyokuwa wamefikiria awali.

Maswikwi alisema watu hao walipiga kelele zilizowafanya watu kukusanyika na kuwaita polisi ambao walifika na kuondoa mwili wa mwanamke huyo katika mifuko, nailoni na maboksi uliyokuwa umefungwa.

"Wakatuambia tuangalie kama tunamfahamu, tulipiga foleni wanawake kwa wanaume, tukamwangalia yule dada (ana umri wa miaka kama 20 hivi), kwa kweli hatukumtambua, hivyo askari wakamchukua," alisema.

Akielezea tukio la pili, Maswikwi alisema majira ya saa 12.00 asubuhi juzi, alipigiwa simu na askari kata akimweleza kuwa kuna msiba katika nyumba ya familia ya Careen Ndondo na hivyo aliamua kwenda eneo la tukio.

"Nilipofika nikakuta kweli amelala mlangoni, wamemfunika kwa shuka, watu wengi wanalia, nikauliza 'vipi?', nikaambiwa kuwa wamemkuta ametupwa hapo alikuwa hana nguo," alisema.

Alisema walimwita mama wa marehemu, ambaye alieleza kuwa mwanawe alikuwa anafanya biashara ya nyanya sokoni, alimtoroka muda kidogo na hakufahamu alikokwenda.

"Alinieleza alikokwenda (marehemu) hajui na wala ndugu zake hawafahamu ila kuna rafiki yake anaitwa Mwache ambaye waliolewa wote Zuzu, ndiye anayefahamu alipo kama kuolewa, kaolewa na nani na ndiye anayetumiwa kuleta matumizi ya mtoto nyumbani," alisema.

Maswikwi alisema walipomwangalia, hakuwa na jeraha lolote mwilini na hivyo hawajui ni nini kilichosababisha kifo chake.

"Yule dada watakuwa wamemuua huko mbali, wakaona waje wamtupe hapa Chinyika inaonekana kama ni ukatili fulani, matukio haya ni mazito. Nitoe wito kwa polisi waongeze juhudi katika kazi yao na hawa watu wakibainika watoe adhabu zinazostahili," alisema.

Mama wa marehemu, Careen Ndondo alisema mwanawe aliondoka wiki nne zilizopita bila kumuaga anakoelekea lakini ilipofika saa 11.00 asubuhi juzi mjukuu wake alimweleza kuwa mama yake mdogo (Alice), amelala kwake na anapomwita haitiki.

"Tukainuka na kaka yake tukaenda pale na kumkuta kalala chali, tukasema msimshike, mtafuteni mwenyekiti lakini alipokuja ndugu yake mwingine alimshika na kumtingisha. Hata hivyo, alimkuta kakauka, nikasema huyu amekufa, siyo mzima," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Theopistha Mallya, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo mawili. Uchunguzi unaendelea.

"Kweli matukio hayo yametokea lakini la huyo mmoja ambaye alifungwa katika kiroba anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 25 hadi 30, hajafahamika, hivyo nitoe wito kwa watu kuja kumtambua ili hatua nyingine zichukuliwe," alisema.

Mapema mwezi huu, katika Kata ya Nzuguni, jijini hapa, wasichana wawili walikutwa wameuawa ndani ya chumba walichokuwa wanaishi baada ya kupigwa na baadaye miili yao kuchomwa moto na watu wasiojulikana.

## Vigogo wa TTCL, UCSAF, Shirika la Posta watenguliwa

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa viongozi wakuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, viongozi

waliotenguliwa ni pamoja na Zuhura Muro, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya (TTCL) na Peter Ulanga, Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo.

Wengine ni Brigedia Jenerali mstaafu Yohana Mabongo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta Tanzania na Maharage Chande, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania.

Rais Samia pia ametengua uteuzi wa Prof. John Nkoma, Mwenyekiti wa Bodi ya UCSAF na Justina Mashiba, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Sharifa Nyanga, Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, haikutaja sababu za kutenguliwa kwa uteuzi wa viongozi hao.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Korti yasimuliwa mama, mwana walivyoua binti

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeelezwa mama alivyomuua mtoto wake, Beatrice Magombola, kwa kumchoma kisu katika titi la kulia kwa kushirikiana na mtoto wake wa kiume, Alphonce Magombola ili asitoe ushahidi mahakamani katika kesi ya nyumba ya familia.

Inadaiwa Machi 16, 2020, saa nne asubuhi, aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni Ramadhani Kingai, alipokea taarifa kutoka kwa msiri kuhusu Beatrice kupotea.

Hayo yalielezwa jana na Wakili wa Serikali Asiath Mzamiru mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo wakati akiwasomea washtakiwa hao maelezo ya mashahidi na vielelezo baada ya upelelezi kukamilika.

Akisoma maelezo hayo, Mzamiru alidai msiri huyo alidai kumekuwa na taarifa za utata kuhusu kupotea kwa binti huyo kwa kuwa mama mzazi wa Beatrice aitwaye Sophia Mwenda, anadai mtoto wake alikwenda Afrika Kusini kwa ajili ya matibabu na wakati mwingine alidai binti yake alikwenda Canada kutibiwa.

Hata hivyo, alidai mama huyo hakuweka wazi ugonjwa unaomsumbua Beatrice na taarifa za ugonjwa hazikuwa zikifahamika kwa ndugu wa Beatrice wala baba yake mzazi isipokuwa kaka yake mkubwa, Alphonce.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa msiri huyo alidai Beatrice alikuwa na gari aina ya Vangard lililokuwa linatumiwa na Alphonce na pia nyumba yake iliuzwa na Sophia na kuna wakati washtakiwa hao wakihojiwa kupotea kwa Beatrice wanakuwa wakali.

"Kutokana na taarifa hizi za msiri, Kamanda Kingai alielekeza kufunguliwa jalada la uchunguzi na upelelezi ulifanyika na kufanikiwa kukamatwa kwa washtakiwa hawa," alidai Wakili Mzamiru wakati akiendelea kusoma maelezo hayo.

Pia inadaiwa kuwa wakati washtakiwa wanachukuliwa maelezo ya onyo, walikiri kumuua Beatrice kwa kumchoma kisu katika titi la kushoto, Alphonce alimfunga miguu na kumshika mikono ndipo Sophia alimchomachoma kwa kisu hadi alipofariki dunia.

"Baada ya kumuua, washtakiwa waliuzungushia shuka mwili na mkeka wa kichina na kwenda kuutupa eneo la Zinga, Bagamoyo," alidai wakili.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa sababu ya kumuua ni kutokana na Beatrice kutaka kwenda kutoa ushahidi mahakamani Mbeya katika kesi ya nyumba ya familia iliyouzwa na washtakiwa hao.

Baada ya upande wa mashtaka kuwasomea washtakiwa maelezo hayo, ulidai utakuwa na mashahidi 40 na vielelezo 13.

Katika kesi hiyo, inadaiwa washtakiwa kwa pamoja walimuua Beatrice Desemba Mosi, 2020 huko Kijichi, Temeke, mkoani Dar es Salaam.

# CRDB yashinda tuzo kimataifa ubora wa kuhudumia wajasiriamali wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

UBUNIFU na umahiri katika mikakati tofauti katika kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja na wadau wengine umeibeba Benki ya CRDB kutunukiwa tuzo ya kimataifa ya benki bora Tanzania inayohudumia biashara ndogo na za kati kwa mwaka 2024 na Jarida la Euromoney la Uingereza.

Tuzo hizo zinazotolewa kwa miaka 30 sasa, huzitambua benki na taasisi za fedha zenye mchango mkubwa kwa jamii inazozihudumia kwa namna tofauti, hivyo kuchangia uchumi wa mataifa yao na dunia kwa ujumla.

"Euromoney ni jarida kubwa duniani linalofanya utafiti wa kina kabla ya kuitambua na kutunuku benki tuzo yake. Wanao uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 30 ya kuandaa tuzo za benki dunia nzima.

"Ninajisikia furaha kwa Benki yetu ya CRDB kushinda tuzo za Euromoney kwa mwaka wa tatu mfululizo sasa," alisema Bonaventura Paul, Mkurugenzi wa Biashara ya Awali na Kati wa Benki ya CRDB aliyepokea tuzo hiyo.

Paul alisema Benki ya CRDB imeongeza juhudi katika kuhudumia wajasiriamali nchini kwa kubuni bidhaa zinazoendana na mahitaji yao, jambo lililowawezesha wafanyabiashara kuimarisha kipato na kukuza miradi yao pamoja na kukuza mchango wao kwenye pato la taifa.

Kati ya juhudi hizo, mkurugenzi huyo alisema ni utaratibu wa kuruhusu wajasiriamali kukopa kwa kutumia taarifa za mtiririko wao wa mzunguko wa fedha za biashara bila kuhitaji kuwa na dhamana.

Mwaka 2023, Benki ya CRDB ilikopesha zaidi ya Sh. trilioni 8.9 na asilimia 12 ya fedha hizo ilielekezwa kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Matumizi ya teknolojia hasa katika malipo, Paul alisema yameongeza ufanisi katika biashara za wajasiriamali wengi. Wajasiriamali wamekuwa wakiunganishwa na mifumo ya kidijitali ya upokeaji na ufanyaji malipo kwa urahisi ikiwamo mfumo wa LIPA Namba na msimbomilia (QR Code), huduma za benki kupitia mtandao na huduma ya SimBanking zinazowawezesha kusimamia kwa urahisi akaunti zao.

Ili kuwafikia wajasiriamali wengi zaidi, Paul alisema benki imetanua wigo kwa kuhusisha wafanyabiashara wachanga ambao nao hunufaika kwa mafunzo na elimu ya fedha inayotolewa kupitia majukwaa tofauti. Hali hiyo, alisema imeifanya benki iongeze fungu inalolitenga kwa ajili ya kundi hili.

Paul aliongezea kuwa katika mkakati wake wa muda wa kati wa miaka mitano 2023 -2027, Benki ya CRDB imetoa kipaumbele kikubwa katika uwezeshaji wajasiriamali wadogo na kati (MSMEs).

Paul alisema katika nusu ya mwaka huu, Benki ya CRDB imeshatoa mikopo yenye thamani ya jumla ya takribani Sh. trilioni 1.5.

Hivi karibuni Benki ya CRDB iliadhimisha Siku ya Wajasiriamali Duniani, ambapo pamoja na maadhimisho hayo, ilizindua akaunti maalum kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati iliyoboreshwa zaidi na inayoendana na mahitaji halisi ya wateja ijulikanayo kama 'Biashara Account.'

Kila mwaka, zaidi ya benki na taasisi za fedha 600 kutoka zaidi ya nchi 100 duniani kote hushiriki tuzo za Euromoney zinazoheshimika zaidi katika sekta ya benki na fedha kutokana na utafiti unaofanywa kuhusu washindi na ushauri elekezi kwa washiriki wote ambao umekuwa msaada mkubwa wa kuboresha huduma za benki nyingi ulimwenguni kote.

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH WILLIUM ROBERT** anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha nne chenye Index No. **S1759/0004/2018** kilichotolewa na shule ya sekondari ILAGALA mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa Polisi: **MWA/MAG/RB/512748/2021**


azamtv

TANGAZO

Ndugu mteja wa AzamTV, Kuanzia Tarehe **1 Agosti 2024** kutakuwa na mabadiliko ya bei kwa baadhi ya vifurushi. Kifurushi cha Azam Plus na Ngorongoro vya **25,000/-** kwa mwezi, sasa vitakuwa **28,000/-** kwa mwezi. Kifurushi cha Azam Pure na Mikumi vya **17,000/-** kwa mwezi vitakuwa **19,000/-** kwa mwezi na Kifurushi cha Azam Lite na Saadani vya **10,000/-** vitakuwa **12,000/-** kwa mwezi.

Kifurushi cha Azam Pure na Mikumi vya wiki vya **6,000/-** vitakuwa **7,000/-** na kile cha Azam Lite na Saadani vya wiki vya **3,000/-** vitakuwa **4,000/-.**

Vifurushi vya visimbuzi vya Antena kwa siku vya shilingi **500/-** kwa siku sasa kitakuwa 600/- na kile cha **1,000/-** kitakuwa **1,200/-** kwa siku.

Vifurushi cha Azam Play na Serengeti vya **35,000/-** kwa mwezi vitabaki vile vile bila mabadiliko.





## Wahukumiwa kifungo miaka 180 gerezani kwa unyang'anyi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imewahukumu watu wawili kutumikia kifungo cha miaka 180 jela kwa makosa sita ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Washtakiwa hao ni Magabe Joseph (22) na Maneno Joseph (24), wote wakazi wa Mtaa wa Mwabasabi, Wilaya ya Geita.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa yote sita pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa vijana wengine wenye tabia ya wizi kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mussa Mlawa, ulipeleka mahakamani mashahidi watano na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa hao walitenda makosa yote sita.

Hakimu huyo alisema washtakiwa wote wawili wametiwa hatiani kwa makosa yote sita. Mahakama ikiwa nafasi ya kufanya maombolezo ili kupunguziwa adhabu.

Washtakiwa wote waliomba kupunguziwa adhabu, wakidai wana familia zinawategemea, pia wazazi ambao wanawategemea.

Wakili wa Serikali Mlawa aliomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria. Hakimu Maweda alisema makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha adhabu yake ni moja tu; haipunguwi na haiongezwi. Matukio hayo yanaongezeka Geita kila kukicha.

Hakimu Maweda alisema Mahakama inawahukumu washtakiwa wote wawili kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kila kosa na adhabu hiyo inakwenda kwa pamoja na wakimaliza kifungo, watakuwa wamejifunza na kuwa raia wema. Rufani iko wazi kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mlawa alidai kuwa Desemba 29, 2022, katika Mtaa wa Nshinde, mkoani Geita washtakiwa wote kwa pamoja waliiba simu mbili aina ya Itel zenye thamani 75,000, fedha Sh. 95,000 na nguo mbalimbali ambapo jumla ya mali zote ni Sh. 170,000. Aidha, mali hizo ni Happiness Mtaswala.

Alidai kuwa kabla au baada ya wizi huo, washtakiwa hao walitumia mapanga kumtishia mlalamikaji ili kujipatia mali hizo.

# Mama, baba mdogo wafariki wakisafirisha mwili wa binti yao

**Na Jaliwason Jasson,** MONDULI

WATU wawili wa familia moja, wakazi wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, wamepoteza maisha kwa ajali ya barabarani, wakati wakitoka kuuchukua mwili wa ndugu yao aliyefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Waliopoteza maisha katika eneo la Monduli jeshini, mkoani Arusha ni ndugu hao wa familia moja waliokuwa wamebeba mwili wa Amina Mnyaruge (42) kutoka mjini Arusha kwenda Babati kwa ajili ya maziko.

Msemaji wa familia hiyo, Issa Mnyaruge, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Maisaka B, Halmashauri ya Babati Mji, alisema jana kuwa ndugu hao walipoteza maisha Julai 20 mwaka huu.

"Mbali na hawa ndugu wa familia moja waliopoteza maisha, wako ndugu wengine wamejeruhiwa vibaya na wanaendelea na matibabu.

"Mmoja wa familia yetu, huyu Amina Mnyaruge, yeye mwili wake ulikuwa ukisafirishwa kuja kuzikwa Babati. Isivyo bahati, gari lililokuwa limebeba mwili likapata ajali na kusababisha vifo vya ndugu zetu wengine wawili," alisema.

Msemaji huyo alieleza kuwa wanafamilia hao wakiwa njiani kutoka Arusha kwenda Babati, gari lao lililokuwa limebeba mwili wa marehemu Amina, liligongana na gari lingine na kusababisha kifo cha mama mzazi wa marehemu Amina na baba yake mdogo, Said Mnyaruge. Miili ya ndugu hao wa familia moja, ilizikwa jana Babati.

Alipotafutwa kuzungumzia ajali hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Justin Masejo, alithibitisha ndugu hao kupoteza maisha katika ajali ya barabarani. Jeshi hilo linachunguza ajali hiyo ili kubaini chanzo chake.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof Kitila Mkumbo, (katikati) akijadiliana jambo na viongozi wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), alipowasili katika ufunguzi wa mjadala kuhusu dira ya taifa ya mwaka 2050, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ma-RC, ma-DC wawekwa kitanzini utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie miradi yote ya maendeleo katika mikoa na wilaya zao na kuhakikisha inakamilishwa ili itoe huduma kwa wananchi.

"Kwenye eneo la usimamizi wa miradi, wakuu wa mikoa hakikisheni mnazo taarifa za utekelezaji miradi hiyo; hii ni fursa yenu ya kujua benki tuliyonayo ya utekelezaji miradi yote ya tangu mwaka 2021.

"Angalieni ni miradi gani imepata fedha, na mjiridhishe kama imekamilika au la, na kama haijakamilika, fuatilieni ni kwanini haijakamilika," ameagiza.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo juzi wakati akizungumza na Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mikoa kwenye kikao kazi alichokiendesha kwa njia ya mtandao akiwa ofisi ndogo ya Waziri Mkuu iliyoko Magogoni jijini Dar es Salaam.

Majaliwa alisema miradi inayojengwa kwa fedha za serikali katika halmashauri na manispaa ni mingi, hivyo akasisitiza ikamilishwe kwa asilimia 90 ifikapo Desemba mwaka huu ili ianze kutumika.

"Matumizi ya miradi hii ndiyo faraja kwa wananchi na ndiyo matamanio yao," alisema Waziri Mkuu, akitumia fursa hiyo kuhimiza viongozi hao wafuatilie uzalishaji chakula ili kuhakikisha Tanzania inakuwa na ziada ya kutosha.

"Tanzania tumezalisha chakula kingi na tuna ziada; wakuu wa mikoa na wilaya jukumu lenu kusimamia kilimo na uzalishaji uwe umefikia malengo na wenye ziada.

"Pia fanyeni sensa ya kujua mazao katika maghala, uhifadhi wake ni mzuri, na je, kinatosha? Tuwe na takwimu za kutosha kuhusu chakula tulichonacho katika hifadhi yetu," aliagiza.

Waziri Mkuu pia alisisitiza makusanyo yote ya fedha katika halmashauri na manispaa ni lazima yaingizwe benki ndipo yapangiwe matumizi.

"Hata kama ni fedha za msaada kutoka taasisi au asasi zisiso za kiserikali, ni lazima DC ajue ili atoe taarifa kwa RC. Ma-RC wasimamie mtiririko wa fedha katika halmashauri.

"Suala la usimamizi wa mapato ya serikali liwe ajenda ya kudumu. Tusipofanya hivyo, tutashindwa kutekeleza mipango yetu.

"Mmemsikia Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan akisisitiza kuhusu ukusanyaji mapato, mapato ambayo baadaye yanaletwa katika maeneo yenu ili kutekeleza miradi," aliagiza.

Maeneo mengine aliyoyawekea msisitizo wakati wa kikao hicho ni pamoja na utatuzi wa kero za wananchi, udhibiti na uhifadhi wa mazingira, nishati safi ya kupikia, ulinzi na usalama, kilimo cha umwagiliaji, magonjwa yasiyoambukiza, maandalizi ya AFCON 2027 na ushirikiano baina ya viongozi wa serikali na wa CCM.

Kikaokazi hicho kilihudhuriwa pia na Waziri wa Nchi (Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uzaji viwanja kupitia vipaza sauti barabarani ni kero

**MTINDO** wa kutangaza biashara ya kuuza viwanja kwa kutumia vipaza sauti barabarani umegeuka kero kwa watumiaji wa barabara hizo. Hivi sasa ukipita katika kila barabara kuu, utakutana na vipaza sauti vilivyopangwa katikati ya barabara hizo vikishindana kutangaza viwanja.

Kwa mfano kwenye makutano ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Sam Nujoma, mataa ya Mwenge kuelekea Barabara ya Bagamoyo, utakutana na vipaza sauti hivyo vikiwa vimepangwa na kuvalishwa nailoni nyeusi, ukiangalia kwa wasiwasi hasa giza linapoingia unaweza kuhisi pengine ni vitoto vimesimama.

Hivi hawa wanaotangaza biashara kupitia vipaza sauti hivyo wanalipa kodi? Kwa sababu tunaelewa kila tangazo ni lazima lilipiwe kodi.

Hiki ni chanzo kingine cha kukusanya mapato ambacho kinaachwa kikipotea na kunufaisha wachache.

Hata kama watangazaji wanalipa kodi, lakini kelele zinazotoka kwenye vipaza sauti hivyo ni usumbufu mkubwa kwa wananchi wengine ambao pia wana haki ya kutumia barabara hizo.

Waziri wa Ardhi, Deogratius Ndejembi, kwanza tunakupongeza kwa kuteuliwa kushika wizara hii na tuna imani kuwa juhudi alizozifanya mtangulizi wako utaziendeleza katika kuondoa kero kwenye wizara yako.

Uuzaji huu wa viwanja kwa matangazo sasa umekuwa ni mtindo kwa kila aliye na viwanja katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Sasa viwanja vinauzwa mpaka kwa kutolewa ofa ya kiwanja kingine iwapo mtu atanunua viwanja zaidi ya kimoja.

Kuna umuhimu kwa wizara husika kuanza kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kupata viwanja halali ili kuwaepusha na matatizo yanayoweza kuwatokea baadaye wanaponunua viwanja hivyo vinavyodaiwa kuwa ni vya ofa.

Kuna kampuni pia ambazo zinanunua ardhi kutoka kwa wamiliki wa ardhi hiyo na baadaye hufanya biashara kwa kuwapimia watu wanaohitaji na kuwaahidi kuwa tayari vina hati.

Aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Jerry Silaa, alianzisha kliniki za kila wilaya kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi na kuelimisha wananchi jinsi ya kupata hati za viwanja vyao.

Hizi kliniki zimesaidia kwa kiasi kikubwa kutoa elimu kwa kuwa wanasheria wa wizara walikuwapo kutoa ushauri na kuelekeza wananchi utaratibu wa kupata haki zao. Wizara, ilipiga marufuku matangazo yote ya kuuza viwanja bila kupata kibali kutoka wizara hiyo mpaka ivihakiki na kuruhusiwa.

Hiyo imetokana na baadhi ya viwanja hivyo kutoendana na vipimo vinavyotakiwa kisheria.

Tukirudi kwenye uuzaji holela wa kutumia vipaza sauti ambavyo muda wote vinapiga kelele barabarani ni uchafuzi wa mazingira unaosababisha kero kwa wengine kwa sababu sio kila mtu anapenda kusikiliza matangazo hayo.

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linapiga marufuku kelele katika maeneo ya umma kwa kuwa ni moja ya uchafuzi wa mazingira.

Hivyo, watu hao pia wanatakiwa wachukuliwe hatua kwa kubughudhi watu wengine.

Wizara ya Ardhi, imefanikiwa kutatua migogoro mingi ya ardhi kupitia kliniki zake ilizoanzisha katika wilaya mbalimbali.

Wananchi wengi ambao walikuwa wakisumbuka kupata hati, kupitia kliniki hizo wamefanikiwa kuzipata na waliokuwa na migogoro wamesuluhishwa na sasa wanaishi kwa amani.

Tuna imani kuwa kliniki zilizoanzishwa zitaendeleza huduma hizo ili kuendelea kutatua kero zinazowasumbua wananchi wengi katika kumiliki ardhi.

Aliyekuwa Waziri wa Ardhi alikuwa mstari wa mbele kusimamia kliniki hizo na kuhakikisha wananchi wanapata haki zao bila usumbufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Miaka minne bila Mkapa, ni mwanadiplomasia aliyeacha alama

**LEO** ni kumbukumbu ya miaka minne ya kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu, hayati Benjamin Mkapa, ambaye alifariki Julai 24 mwaka 2020 na kuzikwa nyumbani kwao Lupaso wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Wakati huu wa kumbukumbu ya kifo chake, naangazia machache kuhusu mwanadiplomasia huyo, hasa kwa kusaidia kuleta suluhu katika nchi za Afrika zilizokuwa na migogoro ya kisiasa.

Mkapa alijihusisha katika harakati za upatanishi wa kieneo ili kuleta amani na usalama katika nchi ya Burundi, kwani alikuwa mwenyekiti wa mkutano wa mazungumzo ya amani ya Burundi akiwaleta pamoja wawakilishi wa serikali iliyokuwa ikiongozwa na Rais Pierre Nkurunziza.

Aliwakutanisha Nkurunziza ambaye naye kwa sasa ni marehemu na wapinzani wake, ili kutafuta suluhisho kwa amani na usalama wa nchi hiyo ambayo ilikumbwa na mgogoro mkubwa wa kisiasa.

Mwanadiplomasia hiyo alichukua hatua hizo baada kuteuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kuwa mmoja wa wasuluhishi wa mgogoro wa kisiasa nchini humo uliokuwa unafukuta.

Mkapa alianza ya usuluhishi mwaka 2015 baada ya kutokea machafuko nchini humo kufuatia Nkurunziza kusema atawania muhula wa tatu na kusababisha mvutano kati yake na wapinzani.

Amani na utulivu nchini humo, ni matunda ya Rais Mkapa na viongozi wengine alioshirikiana nao, hasa baada ya kustaafu na kupata majukumu ya kimataifa ikiwamo kusuluhisha migogoro ya kisiasa.

Ikumbukwe kuwa Mkapa hakujishughulisha na mgogoro wa Burundi tu, bali mchango wake ipo pia nchini Kenya ambako alisaidia kuwapatanisha Raila Odinga na hasimu wake Mwai Kibaki.

Uchaguzi wa urais nchini humo wa mwaka 2007 ulifuatiwa na ghasia kubwa ambazo zilitishia ustawi wa taifa hilo, jitihada zake zilisaidia kuundwa serikali ya mseto na kurejesha utulivu.

Vilevile, Mkapa hakuwa tu akijishughulisha na masuala ya Burundi na Kenya, bali hata mataifa mengine katika eneo la Maziwa Makuu na kujijengea heshima kutokana na mchango wake.

Kwa ujumla ni kwamba, mchango wa mwanadiplomasia huyo, katika masuala mbalimbali ndani na nje ya nchi, ulikuwa bado unahitajika, lakini ametangulia mbele ya haki.

Ni Mkapa aliyepokea kijiti cha urais akawa Rais wa kwanza kuchaguliwa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa uliorejeshwa nchini mwaka 1992 na uchaguzi wa kwanza ukafanyika mwaka 1995.

Kipindi hicho ndicho ambapo 'utitiri' wa vyama vya siasa uliibuka, lakini alifanikiwa kuibuka mshindi na kuongoza nchi kwa mihula miwili akianzia mwaka 1995 na kisha uchaguzi mwingine wa mwaka 2000.

Hata katika kitabu chake cha My Life My Purpose (Maisha Yangu, Kusudi Langu), mwenyewe aliwahi kusema kuwa amezungunzia umuhimu wa utawala bora, demokrasia na jinsi alivyoshirikiana na vyama vya upinzani kwa ajili ya mustakabali wa taifa.

Aidha, ni Mkapa aliyechangia katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania na kupiga vita umasikini kwa kuanzisha mikakati mbalimbali ikiwamo Mkakati wa Kukuza na Kuondoa Umasikini Tanzania (MKUKUTA).

Mkapa aliyekuwa mwanzilishi wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF).

Hakuishia hapo bali alianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na mingine mingi ambayo iliendelezwa na serikali za awamu zilizofuatia baada yake.

Wakati huu wa kumbukumbu ya miaka minne ya kifo chake, hatuna budi kuenzi mema yote ambayo kiongozi huyo alifanya kwa manufaa ya nchi yake na hata nchi za jirani kwa ustawi wa kisiasa

## Jela miaka 30 kwa kunajisi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kabayole, Stephano Fadhili (24) kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kunajisi msichana mwenye umri wa miaka 15.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Joseph Daudi, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasi na kuacha shaka yoyote.

Hakimu Daudi alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kunajisi.

Hakimu Daudi alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Godfrey Odupoy uliipeleka mahakamani huko mashahidi sita na kielelezo kimoja ambacho kilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Daudi alisema siku ya tukio hilo, Agosti 26, 2023, msichana huyo alikwenda kwao na mshtakiwa huyo kwa ajili ya kuchukua fedha za malipo ya kununua dagaa ndipo mshtakiwa alimvuta na kumwingiza ndani ya nyumba na kumnajisi.

Hakimu huyo alisema mshtakiwa ametiwa hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo, ikimpa nafasi ya kufanya maombolezo ili kumpunguzia adhabu.

Mshtakiwa aliomba kupunguziwa adhabu kwa kuwa ana familia na wazazi wake wanamtegemea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Odupoy uliomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Daudi alisema makosa ya kunajisi watoto wadogo adhabu yake ni moja tu, haipunguwi na haiongezeki, na kwamba kutokana na makosa hayo kuongezeka kila kukicha katika Mkoa wa Geita, mahakama inatoa adhabu kali.

Hakimu Daudi alisema mahakama inakuhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na akimaliza kifungo chako atakuwa umejifunza na kuwa raia mwema. Rufani iko wazi kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hiyo.

# Makundi maalum yapewa mbinu za kunufaika na zabuni za serikali

**Na Restuta James**

MENEJA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) Kanda ya Pwani amewataka wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum kujiunga na mfumo wa ununuzi wa umma wa NeST, ili waone zabuni za umma mara tu zinapotangazwa na kuziomba.

Vicky Mollel alitoa rai hiyo juzi wakati wa mkutano wa asubuhi ulioandaliwa na Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) na kukutanisha wanawake na vijana zaidi ya 300.

Alisema wanawake wana nafasi ya kukuza biashara zao kupitia miradi ya serikali kwa njia ya zabuni.

Alisema ili kushinda zabuni, ni muhimu wanawake kujisajili katika mfumo wa NeST ili watambulike na kuwa na uwezo wa kuona zabuni pindi zinapotangazwa.

"Wote mnafahamu kwamba bajeti ya serikali mwaka huu wa 2024/25 ni Sh. trilioni 49.3, asilimia 70 ya bajeti hii itatumika katika ununuzi kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma...

"PPRA inashirikiana na TWCC katika kuhakikisha makundi maalum kama vijana, wanawake, wazee na watu wenye mahitaji maalum wanapata nafasi katika fursa za ununuzi wa umma.

"Kwa mfano, wanawake wana fursa ya kupata asilimia 10 ya zabuni kupitia asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi inayotengwa kwa makundi haya maalum," alisema.

Vicky alisema wanawake wakichangamkia fursa hiyo na kufanikiwa kufanya biashara na serikali, itawasaidia kukuza haraka biashara zao na hivyo kukuza uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, alisema chemba hiyo inalenga kuwezesha wanawake na vijana nchini kuzijua fursa na kuzichangamkia.

Alisema mbali ya mtaji wa fedha, biashara zinahitaji mtandao wa taarifa za masoko, teknolojia ya uzalishaji pamoja na fursa za kukua zaidi.

"Tumekuwa na mikutano hii ya asubuhi kila mwezi, lengo ni kujenga mtandao wa kibiashara, kukutana na wadau wanaowapa fursa wanawake, taarifa na ujuzi ili wafanye uamuzi sahihi katika kukuza biashara zao.

"Leo tumealika watu wa PPRA ambao wameeleza namna ambavyo tunaweza kufanya biashara na serikali," alisema.

Aliongeza kuwa wanawake na vijana wana nafasi ya kuchangamkia soko kubwa la kimataifa (EACLC) Ubungo, ambalo litakuwa na maduka zaidi ya 2,000.

Rais wa chemba hiyo, Mercy Silla, aliwataka wanawake wachangamkie fursa hizo na kujitokeza kwa wingi ili kufaidika na zabuni za umma zinazopatikana.

Aliwataka waingie katika soko la EACLC ambalo litawaunganisha na wazalishaji bidhaa mbalimbali China, wakiwamo wa mashine zinazohitajika kwa wanawake wazalishaji.

Kwa mujibu wa Silla, mkutano huo wa asubuhi ulilenga kuwajengea wanawake na vijana uwezo wa kuingia katika masoko na biashara, kuunda mitandao ya kibiashara na kuelewa soko kubwa la Afrika Mashariki na kufunguliwa kwa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCTA).

Meneja Uendeshaji wa kampuni ya PASS, Neema Nyangalamela, alisema wanawake na vijana walio katika mnyororo wa kuongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo, wanaweza kukopa vifaa na mashine, kuanzia za maandalizi ya shamba, kuvuna na kuzalisha bidhaa kwa ajili ya mlaji wa mwisho.

"Kwenye sekta ya uvuvi tunatoa mkopo wa vifaa kwa wale wanaohusika na mazao yanayolimwa baharini, wafugaji wa wanyama mbalimbali kama kuku, samaki na ng'ombe, wazalishaji asali na wamiliki wa mazao ya misitu," alisema.

Alisema tayari wanachama wa TWCC wameshapatiwa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 50.

Ofisa Masoko wa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT), Pili Kunambi, alisema Watanzania wanaweza kuwekeza na kupata faida kila mwezi katika mfuko huo.



Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya kiraia inayohudumia waraibu wa dawa za kulevya ya Hope and Life Rehabilitation Organization (LHRO) ya mjini Bagamoyo mkoani Pwani, Al-karim Bhanji, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu maendeleo ya awamu ya pili ya mradi wa mwaka mmoja wa kuwawezesha waraibu kutambua haki zao, unaoendeshwa na asasi hiyo kwenye kata tano wilayani humo. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Watatu wafariki dunia, wanane wajeruhiwa basi likigongana na lori

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WATU watatu wamefariki dunia na wengine wanane kujeruhiwa baada ya basi la kampuni ya Zube Trans kugongana uso kwa uso na lori lililokuwa limebeba chupa tupu za soda.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo, akisema kuwa ilitokea juzi saa 12 asubuhi katika Kijiji cha Njirii wilayani Manyoni.

Waliofariki dunia ni pamoja madereva wa basi na lori. Aidha, majina ya waliopoteza maisha kutokana na ajali hiyo hayajafahamika.

Kamanda Lakwale alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni.


Alisema kuwa basi la Zube Trans lenye namba za usajili T 695 DDJ lililokuwa likitokea Mwanza kwenda Dar es Salaam liligongana na lori lenye namba T 908 DVX ambalo lilikuwa likitokea Itigi kwenda mjini Singida.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Furaha Mwakafwila, alisema majeruhi wa ajali hiyo wanaendelea vizuri na miili ya marehemu imehifadhiwa katika hospitali hiyo.

Julai 11 mwaka huu, basi lingine la kampuni hiyo lilipata ajali katika eneo hilohilo la Kijiji cha Njirii.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Mhadhiri wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Mbazingwa Mkiramweni (kulia), akielezea namna vihisia vinavyofanya kazi kwa mmoja wa waliotembelea kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) hivi karibuni. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Dampo linavyohatarisha afya kwa binadamu Pugu

**Na Christina Mwakangale**

DAMPO la Pugu jijini Dar es Salaam ni miongoni mwa eneo lililo na kiwango cha juu cha uchafuzi wa hewa na kuhatarisha afya za binadamu. Utafiti uliotolewa mapema mwaka huu, umebaini.

Eneo hilo lina zaidi ya viwango vya uchafuzi 'Particulate Matter' (PM) 100, ikilinganishwa na viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) cha wastani wa 2.5 na 10.

Pia, kwenye msongamano mkubwa wa magari, shule ya msingi Vingunguti na eneo la DMDP Magomeni, yalibainika kuwa na viwango hivyo vya uchafuzi wa hewa.

Mhadhiri wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Mbazingwa Mkiramweni, aliyasema hayo akihojiana na gazeti hili hivi karibuni kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba katika banda la taasisi hiyo.

Alisema, miongoni mwa majukumu ya taasisi hiyo ni kufanya utafiti, ilibuni mradi wa kupima kiwango na ubora wa hewa jijini na mkoani Dar es Salaam, huku maeneo ya viwandani kwenye makazi pia, hasa usiku yakikithiri uchafuzi wa hewa.

"Utafiti huu ulihusisha kufungwa vihisia maeneo tofauti katika Jiji la Dar es Salaam, kufuatilia ubora wa hewa kwa kutumia vihisia 13 vyenye gharama nafuu vya PurpleAir PA-II vilivyotumika kuanzia Mei 2021 hadi Februari 2022.

"Maeneo yaliyofungwa vihisia ni Pugu Dampo, DMDP Magomeni, Madale, Vijibweni Hospitali, Zahanati ya Buza, Makuburi, Ofisi za Manispaa ya Ubungo na Mlimani City.

"Mengine ni Sinza Hospitali, Ofisi za Manispaa ya Kigamboni, Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, Shule ya Msingi Vingunguti, na Ofisi za Mazingira Wilaya ya Temeke.

Wakati dampo la Pugu ni eneo la wazi la kutupa taka la manispaa, kituo cha DMDP Magomeni kipo karibu na makutano ya barabara, kuna viwango vya juu," alisema mhadhiri huyo.

Alifafanua kwamba mradi huo, ulikuwa ni wa ushirikiano baina ya Taasisi ya Mazingira ya Stockholm (Stockholm Environmental Institute (SEI) Africa Centre, C40 Climate Leadership Group, DIT pamoja na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC) na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

"Mradi ulibuni na kufunga mfumo wa kufuatilia kiwango cha uchafuzi wa hewa kwa jiji la Dar es Salaam, kufanya utafiti wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa hewa na kupitia takwimu zilizopo za uchafuzi wa hewa kutoka kwa vihisia (sensor) vya ardhini na satellite," alisema Dk. Mkiramweni.

Aidha, mradi ulilenga kupima chembechembe yabisi (microscopic solid) ama matone (liquid droplets) madogo, ambayo yanaweza kuvutwa wakati wa kupumua na kusababisha matatizo makubwa ya afya (kwa kifupi/kitaalamu chembechembe hizi huitwa PM2.5 na PM10).

"Kiwango cha PM kikisoma kuanzia sifuri hadi 50 inakubalika. Ila ikiwa kuanzia 50 na kuendelea hadi 100 kwa wale watu ambao wana shida kiafya inawapa shida. Hutakiwi kukaa eneo hilo zaidi ya saa 24, inatakiwa uondoke.

"Pugu Dampo tulibaini 'sensor' zinasoma 100 na kuendelea maana yake mtu akiishi maeneo hayo muda mrefu inaweza kumletea shida. Ila daktari anaweza kufafanua, sisi tumechukua viwango vya WHO.

"Kuna maeneo kama Temeke usiku 'sensor' zinasoma juu pengine kutokana ana viwanda, labda watu wengi wanachoma nyama. 'sensor' hizi tunafunga kilomita moja au isipungue mita 500 kutoka eneo mnalolenga kulitafiti. Kifaa hiki kinatuma majibu muda wote katika simu na popote."

Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mfumo wa Upumuaji kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Mwanaada Kilima, alipoulizwa kuhusu athari za uchafuzi wa hewa kwa binadamu alisema huweza kusababisha magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, kisukari na homoni, ubongo, neva na mfumo wa fahamu, nimonia, macho na mimba kuharibika.

"Kwa ujumla, uchafuzi wa hewa ni kisababishi kikuu cha pili cha maradhi yasioambukiza duniani."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 20 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Siku hiyo ya uzinduzi ndiyo itakuwa siku ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari Mkoani Kigoma, Tabora na Katavi kwa siku saba hadi tarehe 26 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 20 Julai, 2024 hadi siku ya Ijumaa tarehe 26 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 27 Juni, 2024 na:

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**


## Katambi abaini tatizo kutotumika kwa lugha ya alama huduma makundi maalum

**Na Julieth Mkireri**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema kukosekana kwa wataalamu wa lugha ya alama sehemu za kutolea huduma inasababisha baadhi ya makundi maalumu kukosa huduma stahiki.

Katambi amesema ili kundi hilo lipate huduma sawa na wengine mikakati ya kitaifa ya mafunzo ya lugha ya alama kwa watumishi wa umma na watoa huduma tayari hatua zimeanza kuchukuliwa.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya lugha ya alama kwa watumishi wa SUMA JKT jijini hapa na kusema hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023, kuanzishwa kwa mwongozo wa lugha ya alama ambao upo hatua za ukamilishwaji.

Aliipongeza Taasisi ya Foundation for Disabilities Hope (FDH) kwa kutoa mafunzo hayo kwa watumishi hao ambao wanatoa huduma katika taasisi mbalimbali za kutoa huduma kwa watu tofauti wakiwamo wa makundi maalumu.

Pia, alisisitiza waajiri wa sekta mbalimbali za umma na binafsi nchini kuendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo ya lugha ya alama ili waweze kuwasiliana kikamilifu na wananchi wa makundi maalumu wakati wa utoaji wa huduma wanazozihitaji.

Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Uzalishaji Mali wa Jeshi hilo, Kanal Robert Kessy, alisema mafunzo hayo yanakwenda kuwa na mabadiliko kwa watumishi waliohitimu ambao watawasaidia makundi maalumu sehemu za kutolea huduma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya FDH, Malko Hosea, alisema kabla ya kuanza kutoa mafunzo ya alama kwenye maeneo mbalimbali ilifanya utafiti na kubaini watu wenye ulemavu hawapati huduma kikamilifu kutokana na vikwazo mbalimbali.

Hosea, alibainisha baadhi ya vikwazo walivyobaini kuwa ni pamoja na watoa huduma kutokuwa na uelewa wa lugha ya alama na hivyo wenye ulemavu wa kusikia kutopata huduma stahiki.

Utafiti huo pia ulibaini uelewa mdogo kuhusu Sheria namba tisa ya mwaka 2010 na miongozo ya watu wenye ulemavu inayotaka uboreshaji wa huduma za mawasiliano baina ya wenye ulemavu na watoa huduma hali inayosababisha makundi maalumu kupata huduma hafifu.





## Hai wahitaji milioni 65/- kumaliza ujenzi wa shule

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro, Dionis Myinga amesema wanahitaji Sh. milioni 65 kwa ajili ya umaliziaji mradi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame.

Myinga, alisema wamelazimika kuiandikia barua Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kupata fedha za ziada za kuwezesha kukamilika mradi huo.

"Menejimenti imefanya ufuatiliaji wa karibu na kuweka juhudi zaidi katika kusimamia mradi huo ili kuhakikisha kuwa shughuli zilizobaki zinakamilika bila kuchelewa na kupata thamani ya fedha, ambapo bweni moja, vyumba vinne vya madarasa na vyoo matundu sita vimekamilika,"alieleza Myinga.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alitoa mapendekezo sita kuhusu hoja ya kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo iliyopewa na serikali Sh. milioni 372.6.

Mapendekezo ya CAG, ni pamoja na kutaka kuharakisha utekelezaji wa shughuli za mradi ili kuepusha uwezekano wa kuongezeka kwa gharama kwa jumla ya fedha zilizotolewa.

Kuongeza juhudi katika kusimamia miradi inayotekelezwa kwa lengo la kupata thamani ya fedha kwa miradi iliyo ndani ya halmashauri pindi fedha zinapotolewa.

Pendekezo lingine ni kuanzishwa mawasiliano na mamlaka inayohusika ili kushughulikia uwezekano wa kuongezeka kwa gharama zaidi ya matarajio ya awali ili kupata fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha shughuli za miradi.

Limo pia, pendekezo la kutaka kuhakikisha mambo yanayosababisha kuongezeka kwa gharama yanazingatiwa na mamlaka, wakati wa utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya baadae.

Vilevile, CAG alipendekeza kuanzishwa njia za wazi za mawasiliano na mafundi jamii ili kuhakikisha kwamba wanafahamishwa kuhusu hitaji la kuomba kuongezewa muda, iwapo kuna ucheleweshaji wa mradi na kutoa maoni ya kurefusha mara moja ili kuepusha usumbufu na migogoro isiyo ya lazima ya mradi.

# Askofu: Polisi tendeni haki wakati wa uchaguzi S/mitaa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Jimbo la Kilimanjaro Mashariki, Dk. Glorious Shoo, amewataka polisi kutokubali 'Kupofushwa' macho kwa rushwa ili kukibeba chama chochote cha siasa katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Alitoa wito huo wakati akizungumza na askari wanaohitimu mafunzo ya awali ya jeshi hilo katika Shule ya Polisi Moshi, wakati wa mahafali ya dini yaliyofanyika juzi, akiwataka kuwa na hofu ya Mungu.

Mahafali hayo yaliwahusisha askari zaidi ya 300 wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste.

"Kasimamieni haki na kweli kwa kuwasaidia Watanzania kupata viongozi wanaowataka katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji wa Mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025. Kitu kikubwa ambacho mnatakiwa kuishi nacho ni kuachana na utamaduni wa kupofushwa macho kwa rushwa," alisema.

Kadhalika aliongeza kwa kusema: "Wapo askari ambao siyo waaminifu wanaotumiwa na baadhi ya viongozi wenye uchu wa madaraka; jambo ambalo husababisha Watanzania kukosa kiongozi wanayemuhitaji. Kimsingi mambo hayo ndiyo huchochea kukosekana kwa mitazamo chanya na maendeleo katika maeneo wanayoishi".

Pia, alisema: "Mnakwenda huko na mtakwenda kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na Uchaguzi Mkuu mwaka ujao. Tambueni ninyi siyo askari wa vyama vya siasa bali wa Taifa. Hakikisheni mnatenda haki na kusimamia kweli ya Mungu."

Katika mahubiri yake, Askofu Shoo, alisema wako watu wameshauza magari yao, nyumba zao na mashamba ili kugombea kiti fulani na kwenye hizo bajeti na ninyi (askari) mmewekewa, hivyo wanataka kushinda na ni lazima washinde.

Hivyo, kutokana na mpango huo wa wanasiasa wenye uchu wa madaraka, alisema jambo hilo linafifisha na kupofusha ukuaji na ustawi wa nchi.

Alisisitiza ni vyema askari wakajiepusha kupindisha na kuumiza mioyo ya Watanzania kwa kupindisha matokeo kutokana na kitu kidogo wanachopewa.

**Mahafali hayo yaliwahusisha askari zaidi ya 300 wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste.**



Baadhi ya kinamama wa jamii ya Kimasai wa Kata ya Kimokouwa, Wilaya ya Longido mkoani Arusha wakiwa katika mafunzo ya kushona taulo za kike maarufu 'Sodo' kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu wilayani humo juzi, kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la Legal Service Facility (LSF) kupitia mradi wa Wanawake Tunaweza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil.4/- kumaliza kero ya maji Mirerani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAKAZI 57,607 kutoka Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wanatarajia kunufaika na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama baada ya kutaabika kwa miongo kadhaa bila kuwa na huduma hiyo.

Mradi huo unatekelezwa na Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa AUWSA, Justin Rujomba wanatarajia mradi huo utazalisha lita milioni 2.4 kwa siku.

"Maeneo yatakayonufaika ni Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani na kata jirani za Shambarai na Naisinyai. Huu mradi unaigharimu serikali, shilingi bilioni 4.373. Kati ya fedha hizo, Serikali Kuu hadi sasa imeshatoa zaidi ya shilingi bilioni 2.247 na zimeshapokelewa na AUWSA; na utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 75.

"Kazi zilizofanyika mpaka sasa ni uchimbaji wa kisima kirefu, ujenzi wa nyumba ya mashine na uzio, kuvuta umeme, kufunga pampu ya kusukuma maji, kulaza bomba kuu kilomita 10.9 na bomba za kusambaza maji kilomita 48.6, ukarabati wa tanki la zamani lenye ujazo wa lita 150,00, kuunganisha maji kwa wateja 1,100 wa ndani na kuanza ujenzi wa tanki la lita milioni moja," alisema.

Aidha, alisema mradi huo uliibuliwa mwaka 2020 baada ya serikali kubaini upungufu wa maji katika maeneo hayo.


Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alitoa maelekezo kwa AUWSA, kufanya usanifu kwenye visima vilivyochimbwa kupitia mradi mkubwa wa maji jijini Arusha katika maeneo ya Valeska na Mbuguni kwa ajili ya kupeleka huduma ya maji safi Mirerani.

Aidha, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka huu, Godfrey Mzava, aliweka jiwe la msingi katika mradi huo huku akiwapongeza AUWSA kwa namna wanavyoendelea na ujenzi wa mradi huo na kuridhia kuweka jiwe la msingi.

"Ni matarajio makubwa ya jamii ya eneo hili kuwa mradi huu, utakamilika kwa wakati ili wapate huduma ya maji nyumbani kwao na maeneo mengine zikiwemo taasisi mbalimbali," alisema Mzava.

Mkazi wa Kitongoji cha Kilimahewa kilichoko Kata ya Endiamtu, Saumu Bakari, alisema kukamilika kwa mradi huo utafanikisha lengo la Rais Samia Suluhu Hassan la kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema: "Mradi ukikamilika na maji ya bomba yakivutwa kwenye nyumba zetu, kutakuwa na manufaa makubwa kwa jamii hasa wanawake kwa kuwa sisi ndiyo hutumia muda mwingi kufuata huduma ya maji umbali mrefu".



## Mganga Mkuu atoa maagizo matatu kwa watumishi afya

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Jesca Lebba amewataka watumishi wa sekta ya afya mkoani hapa kuhakikisha wanafuata sheria, kanuni na taratibu za kazi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema lengo ni kutoa huduma stahiki na kufikia malengo yaliyowekwa.

Dk. Lebba alitoa kauli hiyo wakati akikabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ambaye kwa sasa amehamishiwa Mkoa wa Dodoma, Dk. Thomas Rutachunzibwa.

Dk. Lebba ambaye amehamishiwa mkoani hapa akitokea Mkoa wa Kigoma aliwataka watumishi hao kutoa ushirikiano na kufanya kazi kwa weledi ili kuzidi kutoa huduma bora katika sekta ya afya.

"Ninajua mna ushirikiano tangu hapo awali lakini tushirikiane zaidi na zaidi kwani tuongeze kasi ya mafanikio na pia tufanye kazi zenye matokeo halisi," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi na wasimamizi mbalimbali wa idara ya afya walioshiriki katika makabidhiano ya ofisi kuendelea kufanya kazi kama timu, akisema kwa kufanya hivyo kutarahisisha kazi.

Aliyekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa alisema ameiacha ofisi katika mikono salama kwani anamfahamu vizuri Dk. Lebba na anaamini katika ufanisi wa utendaji kazi wake, hivyo kutaka apatiwe ushirikiano wa kutosha.

Alisema: "Ninaamini tulishirikiana vizuri sana na ninawaombeni mumpatie ushirikiano wa kutosha Dk. Lebba kama mliokuwa mkinipatia mimi".

**"Ninajua mna ushirikiano tangu hapo awali lakini tushirikiane zaidi na zaidi kwani tuongeze kasi ya mafanikio na pia tufanye kazi zenye matokeo halisi," alisema.**

# Mkandarasi apewa siku tatu kukamilisha mradi

**Na Vitus Audax,** MARA

NAIBU Waziri wa Maji, Kundo Mathew ametoa siku tatu kwa mkandarasi wa kampuni ya Unique Construction Engeneering inayotekeleza mradi wa maji wa Mgango-Kyabakari (Sh.bilioni 70.5) kukamilika ili wananchi wapate maji, vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mathew alitoa kauli hiyo juzi alipokagua mradi huo na kusema kuwa haja ya serikali ni kuona maji yakitoka na wananchi wakipata huduma wala siyo kujua hatua uliofikia kwa asilimia kama ambavyo imekuwa ikitajwa mara kwa mara.

"Mimi ninachotaka ni maji niyaone, kama mlishazoea kiongozi anakuja hapa anatoa maelekezo alafu akiondoka na nyie mnakaa kimya kwangu siyo hivyo nitafanya kambi hapa mtafanya kazi

Mkurugenzi wa mradi huo, Cosmas Sanda alitupa lawama zote kwa mkandarasi huyo kuwa wamekuwa wakimuelekeza mara kwa mara kwa njia mbalimbali zikiwemo barua ili kuharakisha mradi huo lakini kasi yake imeendelea kuwa mbaya, huku akisingizia suala la malipo.

Aidha, Naibu Waziri Mathew alimhoji mkandarasi huyo ili kujua angekamilisha mradi huyo na kuahidi kuwa ifikapo Julai 30 utakuwa umekamilika.

Aidha, mkandarasi huyo (Rafael Mchoma) alitaja sababu ya kuchelewa kukamilika kwa mradi huo ni changamoto mbalimbali walizokuwa wakikabiliana nazo, huku akitaja hatua waliyofikia kuwa na uhakika wa kukamilisha katika muda uliopangwa.




Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, akitoa maelekezo kuhusu ufuatiliaji wa haki za binadamu, uwekaji kumbukumbu, taarifa na usimamizi wa hatari kwa waratibu pamoja na wanachama wa THRDC Kanda ya Ziwa, katika semina ya siku tatu inayoendelea jijini Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wazee wapewa msaada majiko ya gesi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAWAKE wazee katika Manispaa ya Shinyanga, wamepatiwa majiko ya gesi ili kuwasaidia kuondokana na tatizo la macho mekundu pamoja na kutuhumiwa kuwa wachawi kutokana na matumizi ya kuni kwa muda mrefu.

Majiko hayo yalitolewa na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi na kukabidhiwa na Katibu wa Mbunge huyo Samweli Jackson, baada ya kutoa ahadi kwa wazee hao lengo likiwa kuwarudisha katika matumizi ya nishati safi.

Baada ya kukabidhiwa majiko hayo, mmoja wa wazee hao Magreth Maduhu, alisema wamefurahi kupewa majiko hayo ya gesi akisema ni muhimu hasa kwa wanawake wazee kuyatumia

Alisema wataachana na matumizi ya kuni ambayo yamekuwa yakiwasababishia kuwa na macho mekundu na kuanza kutuhumiwa kuwa ni wachawi.

"Ukitumia kuni kupikia lazima uwe na macho mekundu na jamii yetu huku Shinyanga mzee ukionekana una macho hayo unatuhumiwa kuwa ni mchawi, mwisho wa siku wanakuua kwa kukatwa mapanga," alisema Magreth.

Katibu wa Mbunge, Samweli Jackson, alisema wamewapatia wazee majiko hayo kwa ajili ya kutumia nishati safi ya kupikia ili waachane na matumizi ya kuni na mkaa, ambayo huwasababishia kuwa na macho mekundu, pia wawe mabalozi wazuri wa utunzaji mazingira.

Alisema wametoa majiko ya gesi kwa wazee 85 na kwamba tangu waanze kugawa majiko hayo kwa makundi mbalimbali, hadi sasa wameshafikisha kutoa majiko 1,780.

# Zahanati yajengwa kwa miaka 20, haijakamilika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Mwanase Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa zahanati walioianzisha wenyewe miaka 20 iliyopita.

Wananchi hao wamekuwa wakichanga Sh.40,000 kila kaya ili kujenga zahanati hiyo lakini wameshindwa kukamilisha.

Walitoa kilio hicho juzi katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na mbunge wa jimbo hilo, Iddi Kassimu wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hao.

Mkazi wa Kijiji cha Kabondo, Salumu Masasila alisema, walianzisha ujenzi wa zahanati hiyo kuanza msingi wake na wakati huo kulikuwa na halmashauri moja tu ya Wilaya ya Kahama, hakukuwa na Halmashauri za Ushetu na Msalala na sasa yapata zaidi ya miaka 20 bado haijakamilika.

Alisema baada ya kukamilisha msingi mwaka 2011, boma na kuezeka mwaka 2021 tangu mwaka huo haikukamilishwa na halmashauri hali iliyosababisha kuanza kuleta nyufa.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mwanase, Don Leornadi alisema awamu ya kwanza walipokea Sh.milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji na awamu ya pili Sh.milioni 10.

Alisema fedha hizo zipo kwenye akaunti ya kijiji na sasa wameshirikisha kamati ya maendeleo ya kijiji ili kuangalia namna ya kukamilisha ujenzi, kwani wanaingiwa na shaka ya ukamilishaji kwasababu ya nyufa hizo.

Mbunge wa Msalala, Iddi Kassimu alieleza kutokuridhishwa na majibu yaliyotolewa na msimamizi wa ujenzi, kwamba Sh. milioni 50 zilizotolewa awali ya kwanza zilitakiwa kukamilisha ujenzi wake.

Alisema jimbo zima kuna zahanati 34 kati ya hizo ni zahanati moja ya Mwakima iliyokamilika na kuahidi atahakikisha ujenzi wa zahanati hizo unakamilika na kutoa huduma.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hamisi Katimba alikiri zanahati hiyo kuchukua muda mrefu kutokamilika na kuleta nyufa katika kuta kwa sababu ya uzito wa paa ulioezekwa.

Alisema hivi karibuni mradi ulitembelewa na kamati ya fedha ili kuangalia namna ya ukamilishaji wake na kuwaondoa hofu wananchi waliotoa fedha za uanzishaji wake.




**Malipo kidijitali yaonekane kupaisha mapato serikalini**




Dira 2050 itimize maono ya kuwapa wanawake maisha bora aliyokusudia


# siasa

JUMATANO JULAI 24, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU





**BEN MKAPA 1938-2020**

**Mpiganaji anayeishi akizidi kuonyesha njia kujenga uchumi bora na shindani**

BENJAMINI MKAPA-1938/2020

# Ni kiongozi shujaa ndani na nje asiyeweza kusahaulika

**Na Restuta James**

NI miaka minne tangu Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, afariki dunia Julai 24, 2020.

Kumbukumbu ya kifo chake inafanyika ukiwa umesalia mwaka mmoja kumalizika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, aliyoiasisi, ikiwa na kauli mbiu ya kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania.

Katika mahojiano na Nipashe, aliyekuwa mhadhiri mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Donath Olomi, anaelezea safari ya dira hiyo na kazi kubwa iliyofanywa na uongozi wa Mkapa.

Anasema miongoni mwa malengo ya Dira 2025, ilikuwa ni kuwa na taifa la watu walioelimika na wanaotafuta maarifa kupitia elimu.

"Juhudi zimefanyika, changamoto ni kwenye ubora wa elimu. Watu wengi wanasoma hadi chuo kikuu lakini kiwango cha uelimishaji nina mashaka siyo kile tulichokitaka kwenye dira," anasema.

Anaongeza kuwa dira ilitamani Tanzania ya watu walioelimika na wanaojielimisha, wanaotumia sayansi na teknolojia kujiendeleza na kufikia uchumi wa kati.

"Utafutaji wa maarifa bado sana. Ni mojawapo ya eneo linalohitaji kufanyiwa kazi. Tunaona watu wanasoma ili kupata vyeti lakini ile tabia ya watu kujielimisha bado. Ni eneo la kuwekewa mkazo kwenye Dira 2050."

Akiangazia zaidi sekta hiyo, Dk. Olomi anasema imepanuka sana ikilinganishwa na mwaka 2000, akitaja ongezeko la shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu.

"Tumewekeza kwenye miundombinu ni jambo muhimu sana. Lakini kubwa zaidi katika ukuzaji wa jamii na uchumi elimu inayopatikana iwe bora," anasisitiza.

Dk. Olomi ambaye ni mtaalamu wa uchumi, anafafanua kuwa iwe ni elimu inayompa kijana maisha siyo matarajio bila kumpatia zana za kuweza kupambana na maisha na zama hizi ambazo tatizo kubwa la ajira, hivyo elimu imwezesha kijana kujitafuta.

"Katika kutafuta maarifa bado sana. Ni moja ya eneo linalohitaji kuwekewa mkakati kwenye dira 2050 ili tuweze kuwa na taifa la watu walioelimika, wenye maarifa yanayowasaidia wao na dunia," anasema na kuongeza kuwa elimu iwafanye watu kusoma na kuelimika siyo kupata vyeti.



Benjamin Mkapa na Rais wa Afrika Kusini Nelson Mandela (kulia) enzi za uhai wao, wakiwa Dar es Salaam, mwaka 1998. **PICHA: MTANDAO**

**MAISHA BORA**

Akizungumzia suala hilo, anasema dira inayotimiza miaka 25 mwakani, pamoja na mambo mengine, ililenga kumletea kila Mtanzania maisha bora na kufungua uchumi wa soko ili bidhaa zipatikane kwa unafuu na kiushindani.

"Siyo uchumi wa kati tulionao... dira ilitaka tuwe juu yake. Hatujafika na mwaka kesho ndio tunamaliza miaka 25, lakini naweza kusema tunapopanga kujiwekea malengo ni lazima yawe makubwa, japokuwa kwenye utekelezaji tunaweza tusiyafikie," anasema, akigusia kuwa Tanzania ingeweza kuwa mbali zaidi kuliko hapa ilipofikia.

Anagusia miundombinu ya usafiri na usafirishaji pamoja na huduma za kijamii kama afya, kuwa inahitaji kuimarishwa zaidi dira ijayo, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na mtangamano wa watu na bidhaa yakiwamo mazao na malighafi kutoka sehemu zote za nchi.

Dk. Olomi anasema Tanzania imeendelea, vijijini kuna mabadiliko makubwa zikiwamo nyumba za kisasa, zenye umeme na pia nchi imejitosheleza kwa chakula.

Hata hivyo, anasema mkazo unapaswa kuwekwa ili utoshelevu wa chakula uondoe udumavu kwa watoto, utapiamlo na lishe duni kwa wote.

Takwimu za serikali zinaonyesha kuwa kiwango cha udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ni kikubwa huku Njombe ukiongoza kwa asilimia 50.4, ikifuata Rukwa kwa asilimia 49.8 wakati kiwango cha kitaifa ni asilimia 30 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 34 mwaka 2015.

**UTAWALA BORA, RUSHWA**

Kuhusu utawala bora, anasema ili uonekane katika ngazi zote, ni lazima kutokomeza rushwa.

"Rushwa inakwenda na jinsi ambavyo tunafanya siasa, ikishaanzia kwenye siasa hakuna wa kuipiga vita. Ni tatizo kubwa sana linakwaza uchumi na sekta zote pia usalama wa nchi," anaonya Dk. Olomi, ambaye alikuwa mmoja wa wataalamu walioandika Dira 2025.

Anasema rushwa ni pamoja na 'wananchi masikini' kuchanga fedha za kununua 'wapigakura' wakati wa mchakato wa uteuzi.

Akizungumzia uchaguzi huru na wa haki, anakumbusha kauli ya ushindi 'nje ya boksi' iliyotolewa na aliyekuwa Waziri Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliyeahidi kwamba angemsaidia Mbunge wa Bukoba Mjini (CCM), Stephen Byabato, ashinde ubunge mwakani kwa madai kuwa ushindi wa uchaguzi hautegemei wingi wa kura kwenye boksi bali anayehesabu na kutangaza matokeo.

Uteuzi wa Nape umetenguliwa na CCM imejitenga na kauli hiyo kwa kueleza kuwa itaheshimu matokeo halali ya chaguzi zote ukiwa wa serikali za mitaa mwaka huu na mkuu mwakani. Dk. Olomi anaonya: "Watu wanasikiliza na wanajazwa presha ya hasira kidogo kidogo, mwisho linakuwa jambo baya kwenye nchi yetu."

Kuhusu matumizi ya rasilimali, Dk. Olomi anashauri katika miaka 25 ijayo, dira mpya isisitize tathmini na namna ya kuzitumia ikiwamo matumizi ya dawa za asili na uhifadhi wa lugha na maarifa asilia kwa manufaa ya nchi na dunia.

**MKAPA/DIRA 2025**

Mkapa aliongoza nchi kuanzia 1995 hadi 2005 na katika kipindi hicho, aliandaa na kuanza kusimamia utekelezaji wake. Alifariki dunia Julai 24, 2020 jijini Dar es Salaam alipokuwa akitibiwa.

# Malipo kidijitali yaonekane kupaisha mapato serikalini

Na Dk. Felicia Kilahama

MWAKA wa fedha 2023/2024 umemalizika serikali ikitarajia kutumia Shilingi trilioni 49.35 kutimiza mipango mbalimbali ya maendeleo kwa bajeti iliyoanza mwezi huu.

Kwa ujumla hiki ni kiasi kingi cha fedha wananchi wanategemea mafanikio mengi yatakayoboresha huduma za afya katika kipindi hicho kilichoanza Julai 1, 2024 hadi Juni 30 mwakani.

Pamoja na ongezeko la bajeti 2024/2025, bado ni mipango na utekelezaji rasmi utategemea upatikanaji wa kodi na mapato mengine ya serikali, kwenye hazina chombo mahususi kinachosimamia masuala ya mapato na matumizi ya fedha za serikali.

Kwa kushirikiana na vyombo vingine hususani Benki Kuu, TRA, serikali za mitaa na taasisi za umma.

Bunge pia kupitia kamati zake za kisekta, huwajibika kufuatilia matumizi ili yaendane na kile kilichopitishwa ukiwamo muswada wa fedha ambao ukisainiwa na Rais, unakuwa sheria ya fedha ili makadirio na matumizi ya fedha yapate nguvu ya kisheria.

Katika kutekeleza bajeti hii serikali inasisitiza kuweka mkazo wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki ikiwa ni pamoja na kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) (ICT), kukusanya mapato.

Pia kutumia mfumo wa serikali wa kielektroniki wa malipo ya (GePG) kwa wizara na taasisi nyingine pamoja na namba ya udhibiti katika miamala yote ya kiserikali na matumizi zaidi ya mashine za kielektroniki za EFD, ili kuongeza ufanisi wa kukusanya kodi na tozo mbalimbali.


Hiyo ni mifano michache ya ambayo kiuhalisia ikitumiwa vizuri inaweza kuongeza mapato ya serikali kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji ya taifa kila mwaka bila kuhangaika kukopa. Hata kwa kulazimika kukopa iwe ni wa kiasi kidogo,

Tunajiuliza tunakopa kila mwaka ili kufanya kitu gani cha lazima? Iwapo nia ni kutaka Watanzania waende kwenye mwezi, wengi tutasema hilo siyo hitaji la msingi kulazimika kukopa.

Lakini vipaumbele vya taifa vikiwa vyenye kuinua maisha ya wengi serikali ikope, iwapo nguvu zimepwaya na pawepo sababu za kuridhisha.

Hata hivyo, kufanya kazi kwa bidii na kila Mtanzania kuwajibika ipasavyo; nchi ina utajiri mwingi rasilimali kama ardhi na watu ili kufikia maendeleo.

Kiuhalisia taifa bado liko kwenye kuhangaikia maendeleo halisi na endelevu kwa wananchi wake. Kwa kiasi fulani limepiga hatua lakini bado hali ni tete na



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: MTANDAO**

> “Serikali iwe macho kuhusu matumizi ya kielektroniki, na panapogundulika ubadhirifu, hatua kali kiutawala na kisheria zichukuliwe bila kukawia na kwa misingi ya uwajibikaji.

hasa ikizingatiwa ukubwa wa nchi na ongezeko la watu pamoja na mifugo.

Taifa fulani, linaweza likasifiwa kwa kuwaletea maendeleo watu wake lakini ukiangalia ukubwa wake na namba ya watu bado utaona kuna tofauti na nchi yenye eneo kubwa kama Tanzania.

Mathalani, taifa lenye eneo dogo rasilimali zake pia ni haba ukilinganiswa na lenye eneo kubwa kama Tanzania, yenye rasilimali tele tena ikipatikana na Bahari ya Hindi kwa zaidi ya kilomita 1,000, ikimiliki rasilimali zilizomo ndani ya ukanda wa kilomita 200 baharini kutoka ardhi inapoishia.

Kuna mikoko takribani hekta 150,000, zenye ikolojia ya kuzalia samaki na viumbe bahari wengine wengi.

Kimsingi mapato ya serikali yanatokana na wananchi na wawekezaji kwa kulipa kodi, kadhalika, uwezo wa kulipa kodi ni kutokana na kipato kinachotokana na matumizi ya ardhi kuzalisha mali kupitia kilimo na ufugaji, matumizi mbalimbali ya maliasili zilizopo na biashara.

Pia, upo utalii, ujasiriamali, uwekezaji wa namna mbalimbali na huduma. Watanzania tunapoiweka serikali madarakani tunatarajia itumikie na kutuletea maendeleo tunayotarajia.

Kwa upande mwingine ni wajibu wetu kuhakikisha tunaiwezesha kwa kulipa kodi na tozo kufanikisha utekelezaji wa mipango kupata maendeleo tunayoyatarajia.

Wengi tungependa kulipa kodi ili ndoto zetu kimaendeleo ziweze kutimizwa, mathalani, tumeshuhudia wengi wakimiminika kutumia usafiri wa relimwendokasi ya SGR kwenda Morogoro ikiwa ni ishara njema ya matokeo ya juhudi za serikali.

Kwa uzoefu tulionao changamoto za kulipa kodi zimekuwa zikijitokeza sababu viwango vya kodi na tozo pamoja na ukusanyaji unavyofanyika; lakini siyo kuwa watu hawataki kulipa.

Kadhalika, walipakodi wanapokuwa hawaoni kinafanyika kunajitokeza sintofahamu kwamba nalipa kodi ili iweje? Iwapo matumizi ya fedha hizo yanapokuwa hayakisi viwango vya maendeleo; kunakuwapo na vinyogo kwenye kulipa lakini haitekelezi kilichotarajiwa kutokana na ubadhirifu au upotvu wa fedha za umma kwa kukosa usimamizi madhubuti.

Ni imani yangu kuwa iwapo kutakuwapo na usimamizi madhubuti na uwajibikaji wa pamoja na viwango vya kodi na njia za makusanyo pia zikawa rafiki, hakuna shaka wengi watapenda kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yao.

Ikumbukwe watu wengi tunaoishi mijini maisha yanategemea bidhaa za madukani yawe madogo kwa makubwa -‘supamaketi’ pia kwenye masoko ya bidhaa za shambani na viwandani kama Kisutu Dar-Es-Salaam, Kingalu, Morogoro na Mwanjelwa Mbeya.

Wanaouza bidhaa madukani wanatakiwa watumie mashine za kielektroniki za EFD, TRA inasisitiza, “ukinunua dai risiti; ukiuza toa risiti.”

Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwapo kukengeuka kuhusu matumizi ya mashine hizo muhimu za kufanikisha kupata mapato.

Ukinunua bidhaa kwenye maduka makubwa mpokea fedha anapofungua sehemu ya kuweka fedha, hapohapo risiti inajitokeza kupitia mfumo uliounganishwa na kompyuta ya mauzo.

Risiti inaonyesha mchanganua wa kiasi kilicholipwa na VAT anayokatwa kulingana na thamani ya bidhaa alizonunua na ndipo ‘dai na toa risiti’ inapofanikisha.

Kwenye biashara za mitaani, na maeneo mengine yenye mikusanyiko mikubwa ya wajasiriamali na wateja wengi mijini na majijini, matumizi ya utaratibu kama huo si kwa viwango tarajiwa. Walio na EFD ni wachache, utaratibu wa kudai risiti ni kero mno hadi kununiana.

Tatizo ni kukwepa VAT muuzaji akisema usipodai risiti bei ni kiasi fulani ukidai risiti utalipa zaidi mteja atakubali kulipa bila risiti.

Tusidanganyane kwa asilimia 18 VAT inayotozwa uzalendo haupo. Ikipungua kwa kiwango ambacho kitawafanya Watanzania kuwa wazalendo haina shida hata wauzaji watapata bidhaa kwa gharama nafuu, muuzaji na mteja tupata risiti bila vikwazo.

Vilevile, tutasema ‘watumishi wa TRA ni wenye ukwasi’ hata kama mishahara yao ni mikubwa, tukumbuke ni binadamu wenye udhaifu kama wengine.

Pia dunia imezingirwa na bidhaa nyingi, hatarishi na za kutamanisha ‘kupindukia’. Bila kuimarisha mifumo ya kielektroniki, pamoja na sera, sheria na kusimamia ipasavyo; serikali itaendela kupoteza fedha nyingi hata kama kutakuwapo na miamala mingi.

Matumizi ya kielektroniki pamoja na miamala kupitia mashine zinazotumiwa na binadamu, ni rahisi kughushiwa.

Wataalamu wanaohusika, kwa ujanja wanao uwezo wa kutoa miamala batili yenye kuwanufaisha wachache badala ya wengi maana miamala halisi haitawasilisha fedha hazina.

Kwa msemo wa mitaani fedha ya umma inapigwa kiwiko pia inachukua muda mrefu kugundua udanganyifu hivyo, hasara inakuwa kubwa kiasi cha kuzorotesha huduma za kijamii na maendeleo yanayotarajiwa.

Serikali iwe macho kuhusu matumizi ya kielektroniki, na panapogundulika ubadhirifu, hatua kali kiutawala na kisheria zichukuliwe bila kukawia na kwa misingi ya uwajibikaji.

MKAPA 1938-2020

# Dira 2050 itimize maono kuwapa wanawake maisha bora aliyokusudia

**Na Mwandishi Wetu**




Wanawake wakifurahia mafanikio wakati wa kongamano la kuchangia maoni ya uandishi dira mpya 2050. **PICHA: MWANDISHI WETU**

RAIS Benjamin Mkapa ni moja ya viongozi waliokuwa na nia ya kuibadilisha Tanzania ili kufikia maendeleo endelevu na hata msamiati 'endelevu', ulioanza kusikika wakati wa uongozi wake.

Ndizo zama msisitizo wa matumizi ya sayansi na teknolojia, maisha bora, ushirikishwaji jamii na uchumi shindani ulipopata msukumo zaidi.

Taifa linapomkumbuka Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Mkapa, linaendelea kutoa maoni kuandaa dira ya maendeleo ya 2050, baada ya kutekeleza dira ya 2025, iliyotayarishwa wakati wa uongozi wake.

Ili kuandaa dira na uelekeo mwingine wa taifa, wadau mbalimbali wakiwamo wanawake ambao idadi yao ni kubwa zaidi, wanachambua dira inayoelekea ukingoni na kuona jinsi inavyotakiwa kufanyiwa maboresho ili ijayo iwe ya usawa wa kijinsia na ilete maisha bora kwa wote Mkapa aliyoyatamani.

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, mwakani inafikia ukingoni na kikubwa ilikuwa na uelekeo wa kukuza biashara ya mauzo ya nje na kuongeza au kuimarisha ushindani wakati inamalizika.

Wanawake wanaotoa maoni kuhusu utekelezaji wa dira hiyo wanaangazia uhalisia wa maisha bora kwa kila Mtanzania na iwapo idara iliwanufaisha.

Wanaainisha kuwa katika kuandaa Tanzania bora na maisha mazuri, wmeachwa nyuma kiasi kwamba umaskini wa taifa umevikwa sura ya mwanamke maskini wa kijijini.

Wanaona kuwa wanawake wamezidi kuwa na maisha duni japo ndiyo washiriki wakuu wa uzalishaji mali na chakula na kulifanya taifa kujitosheleza kwa chakula asilimia 120.

Rose Marandu, ni Mkurugenzi wa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake (TWF), unashirikiana na wadau wakiwamo Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP kufanikisha kongomano la kitaifa la kukusanya maoni ya wanawake kuelekea uandishi wa dira mpya 2050.

Rose anasema asilimia 51 ya wanawake wameachwa kwenye uzalishaji wa kisasa, wakibakia ndani ya sekta isiyo rasmi tena ni wachuuzi, wafanyabiashara ndogondogo zisizo na mitaji wala sifa ya kukua.

Akizungumza kwenye kongamano hilo hivi karibuni, anaeleza kuwa hawana mikopo, badala yake wanategemea ile ya vikoba na kaushadamu ambayo siyo fedha nyingi za kukuza wala kupanua biashara zao.

Aidha, kwa kuangalia dira hiyo inayomaliza muda wake anagusia suala la chakula kuwa licha ya taifa kujitosheleza kwa chakula, udumavu wa watoto wa chini ya miaka mitano ni mkubwa.

Anasema udumavu na utapiamlo ni tishio hata katika mikoa wazalishaji wakuu kama Njombe na Katavi kiwango kikizidi kile cha taifa.

"Licha ya kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 130 mwaka 2024/25 kwa mujibu wa Wizara ya KIlimo, asilimia 20 ya familia hazina uwezo wa kumudu chakula cha kutosha chenye virutubisho cha kuwawezesha kuwa timamu na kushiriki maendeleo ya nchi."

Akizungumzia elimu ambayo pia ni takwa la dira hiyo ya 2025, anasifu juhudi za kuongeza usawa wa kijinsia katika kuandikisha na kudahili wanafunzi shuleni na vyuoni.

Idadi yao imeongezeka kuanzia shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu, anasema.

Kwa mfano, Rose anasema mwaka 2017 usajili wa watoto shule za msingi ulifikia asilimia 89.6 wasichana wakati wavulana walifikia asilimia 86.

Kadhalika, kiwango cha kujiunga na vyuo vikuu idadi ya wanawake imeongezeka na kufikia asilimia 34.5, hata hivyo ana angalizo kuwa utoro, mimba za utotoni na unyanyasaji kijinsia.

Anasema pengo la kijinsia linaonekana kwenye dira inayomaliza muda wake kwa sababu watoto wengi wanaotakiwa kuwa shuleni hawako darasani kutokana na unyanyasaji kingono na utumikishwaji kwa upande wa wavulana.

Rose anasema wanawake wanataka makosa hayo yarekebishwe ili elimu bora ipatikane isiwe 'elimu cheti' bali kupata maarifa ya kupambana na mabadiliko na changamoto za dunia ya sasa na kubadilisha maisha ya wanawake.

Rose anakumbusha kuwa dira inayomaliza muda haikuweka usawa wa kijinsia kuwa suala mtambuka mbali na kulitaja kwenye maisha bora kwa kila Mtanzania. Anasisitiza bado uwakilishi wa wanawake kwenye uongozi na siasa haujakaa sawa wanapata nafasi kwenye bunge kupitia viti maalumu na siyo mambo jumuishi ya kuhakikisha taifa linafikia uwakilishi wa 50/50.

Kadhalika, wanawake wanaona kwamba mchakato wa kupata viti maalumu siyo wa uwazi, lakini japo unawapa ubunge unawanyima nafasi za kuwa Waziri Mkuu na pia kupata fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo.

Akichambua pengo la usawa wa kijinsia kwenye kumiliki rasilimali, ajira na kuwa na uwezo wa ushindani kwenye dunia ya sasa, Mkurugenzi wa WFT, anasema

"Dira haijawezesha wanawake kumiliki rasilimali kwa mfano ni asilimia nane pekee wanaomiliki ardhi. Ajira ni shida, walioajiriwa sekta ya umma ni wachache sana na yote hayo yanahitaji kufanywa upya kwenye dira ijayo."

Aidha, "Takwimu zinaonyesha kuwa kwenye kilimo wanawake ni asilimia 54, wanaume ni 44, kwenye ajira sekta ya umma ni asilimia 48 wakati wanaume ni asilimia 68, kwenye mashirika ya umma ni asilimia 18 pekee. Tunajiuliza ajira zinapatikanaje? Kuna vikwazo gani...? Anahoji Rose.

> Udumavu na utapiamlo ni tishio hata katika mikoa wazalishaji wakuu kama Njombe na Katavi kiwango kikizidi kile cha taifa.

Akizungumzia umiliki wa rasilimali anasema asilimia saba pekee ya wanawake wanamiliki nyumba, wakati asilimia 28 wanamiliki kwa ubia na wanaume jambo linaloongeza hofu kuwa mwanaume akifariki mama anaweza kufurumushwa.

Pia, anasema wanawake asilimia nane pekee wanamiliki ardhi lakini ndiyo wanazalisha mali na wanaolilisha taifa.

**UONGOZI / UTAWALA BORA**

Rose anazungumzia utawala na uongozi ambako dira ilitamani kila Mtanzania awe kiongozi na ashiriki kwenye kuendeleza taifa na kupiga vita rushwa na uwajibikaji. Wanawake wameongezeka katika uongozi lakini bado idadi yao ni asilimia 27 kwenye ngazi za juu.

Katika kushiriki uongozi ndani ya jamii hasa kuufikia uongozi kupitia uchaguzi jimboni, mitazamo hasi na rushwa ya ngono imewakwamisha kuchaguliwa.

Kwa ujumla wakati huu wa kuangalia kazi na huduma ya Mkapa katika maendeleo ya taifa suala la kuwa na dira yenye mtizamo wa kijinsia ni muhimu ili kila Mtanzania mtoto hadi mzee, mwenye ulemavu na viungo kamili afikie maisha bora hayati Mkapa aliyoyatamani kuwapatia ifikapo 2025.

## BEN MKAPA 1938-2020

# Mpiganaji anayeishi akizidi kuonyesha njia kujenga uchumi bora na shindani

**Na Gaudensia Mngumi**



Rais mstaafu, hayati Benjamin Mkapa.

NI miaka minne tangu kifo cha Rais mstaafu Benjamin Mkapa, maarufu Ben aliyetwaliwa Julai 24, 2020 akiwa na miaka 82.

Msomi huyo wa Chuo Kikuu cha Makerere -Uganda, anakumbukwa kwa jitihada kubwa za kuboresha na kuinua uchumi wa Tanzania akiingiza kwenye uchumi shindani wa soko huria.

Katika kuboresha na kufufua uchumi alijaribu mbinu nyingi ikiwamo kubinafsisha mashirika mfu ya umma ambayo tangu ayabinafsishe imetimia takribani miongo miwili sasa.

Wengi wanamkumbuka Ben katika eneo la ubinafsishaji, akitwa dalali wa kuuza mashirika hayo.

Leo Jukwaa la Uongozi, linamkumbuka kwa kutazama jitihada zake hizo lakini kwa kuangalia historia, changamoto na mafanikio hata kile ambacho kinaweza kufanyika ili mashirika yaliyobaki yachangie maendeleo ya nchi.

Tukirejea juhudi zake ni wazi kuwa Mkapa alifanyakazi ya kurejesha uchumi katika hali bora baada ya kuyumba katika miaka ya nyuma kuanzia 1970.

Ben anakumbukwa katika juhudi alizofanya kutatua tatizo la mashirika kuwa mzigo mzito kwa serikali na Watanzania tangu awamu ya kwanza.

Pengine katika tafakuri hiyo ya kubadilisha sura ya mashirika hayo wapo watakaoibuka na mitazamo mbalimbali mfano, Mkapa alifanya vizuri, kuna upungufu au kungekuwa na mbadala.

Itakumbukwa alirithi, changamoto zilizoanzia awamu ya kwanza iliyoongozwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. Ndiyo iliyojenga viwanda vingi na kuifanya Tanzania kuwa moja ya mataifa yenye viwanda vingi Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara.

Lakini hata hivyo, wakati Nyerere anaondoka madarakani au kung'atuka, viwanda vingi vilikuwa taabani.

Sababu nyingi zinaainishwa kama ukosefu wa fedha za kigeni uliotokana na mdororo na kuyumba biashara duniani zikiwamo za mazao na mali ghafi kutoka Afrika na Tanzania pia.

Kuyumba soko hilo kuliifanya Tanzania kukosa fedha za kigeni kutokana na biashara ya mazao kutikisika katika soko la dunia na wakati huo fedha za kigeni zilitoka serikalini pekee kwa kuuza mazao mbalimbali na zilipatikana Benki Kuu (BoT) pekee.

Kadhalika, kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kuliongeza kukwama kiuchumi na shughuli za uzalishaji, kukiirudisha nyuma nchi ambayo ililazimika kuanza upya kujenga uchumi wake.

Kwa mfano, ililazimika kuunda mashirika yake yenyewe mfano la reli na ndege na kununua vitendea kazi na kufunza wataalamu, yote hayo yakigharimu dola na rasilimali nyingine nyingi.

Aidha, vita ya Kagera ilisababisha hasara kubwa kwa taifa na kukosekana fedha za kigeni na za ndani kwa sababu kila senti ilielekezwa kulinda mipaka yake.

Ndiyo maana wataalamu wa uchumi na biashara wanaeleza kuwa kuwapo kwa changamoto hizo za kiuchumi za ndani na nje ya nchi miaka ya 1970 kulichangia mashirika hayo kufa.

> Ben mwenyewe katika kitabu chake, alikiri kuwa mwenendo wa ubinafsishaji mashirika ulikuwa na changamoto na alikiri upungufu.

### UFISADI/ KUKOSA UTAALAMU

Kukosekana wataalamu wa kuendesha, mashirika hayo kusimamia uendeshaji, uzalishaji, mauzo, kutunza fedha na kufuatilia faida ni chanzo kingine cha mashirika kufa.

Hata hivyo, kulikuwa na ufisadi, watu waliiba ndani ya taasisi hizo misemo kama ya umma haiumi ilitamalaki. Pia kulikuwa na kuzalisha bidhaa kiasi kidogo ili zikosekane na kuwe na uhaba mkubwa ili baadhi ya watumishi wazilangue na kutajirika.

Miaka hiyo, mfano simenti ilikuwa ikizalishwa kiasi kidogo ili walanguzi wapate nafasi ya kuiuza sokoni hivyo kuzuia uzalishaji wakilenga kujinufaisha, yote ni sehemu ya ufisadi katika sekta hiyo.

Itakumbukwa, Rais Ali Hassan Mwinyi, alipoingia madarakani alikuta hali mbaya ya mashirika, yakiwa hoi, lakini kutegemea ruzuku ya hazina.

Baada ya kusaini mikataba na mashiriki ya fedha ya kimataifa, Tanzania ililazimika kutekeleza masharti kadhaa ikiwamo kubinafsisha mashiriki, kuondoa ruzuku, serikali kujiondoa kwenye uzalishaji na umiliki wa mashirika, kufungua milango ya soko huria na kuipa sekta binafsi kipaumbele kuendesha uchumi.

### UDHAIFU UBINAFSISHAJI

Ben mwenyewe katika kitabu chake, alikiri kuwa mwenendo wa ubinafsishaji mashiriki ulikuwa na changamoto na alikiri upungufu.

Hata hivyo ukweli ni kwamba utekelezaji wake ulifanyika kwa shinikizo na presha za mashirika ya kigeni, tena kwa muda mfupi.

Kwa ujumla hakukuwa na muda wa kutosha wa kupanga, kuandaa mikataba, kuweka mipango kabambe na kuwa na utaalamu wa uliohitajika kabla ya ubinafsishaji huo.

Licha ya kwamba nia ilikuwa nzuri kuwa taifa litakuwa na viwanda, bidhaa za kutosha, kodi na tozo kwa wingi na ajira kwa vijana yote yakichangia maendeleo ya nchini mambo hayakwenda kama ilivyotarajiwa.

Kuna baadhi ya mashirika yamefanikiwa mfano benki ya NBC ilipovunjwa kuunda NMB, imekuwa na tija na benki hiyo imesambaa nchi nzima hata kuizidi NBC wakati wa awamu ya pili na ya kwanza.

Kadhalika, vipo viwanda vichache vimefanya vizuri, lakini vingine vingi vikiwamo vya nguo, nyama (Tanganyika Packer} Mashine Tools Moshi, General Tires, Karakana ya Mang'ula na vingine vingi 'vimeangamia'.

### MABADILIKO KISERA

Ikumbukwe baada ya Tanzania kuingia mikataba na mashirika kama Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha la Kimataifa, IMF, sera za kiuchumi nazo zimebadilika, hakuna tena sheria na sera za kulinda viwanda vya ndani.

Hali hiyo imesababisha viwanda vilivyobinafsishwa kushindwa kuzalisha, kwa sababu soko liko huru bidhaa za kila aina ziko sokoni, haviwezi kushindana na haviwezi kuzalisha kifaida.

Mfano, viwanda vya nguo, maturubai, redio, betrii, matairi na viatu, vimepambana na ushindani mkubwa zaidi kwani bidhaa za kila namna za aina hiyo toka nje ziko kwa wingi nchini.

Tena hupatikana kwa bei nafuu kuliko zile ambazo zingezalishwa ndani, yote hayo ni baada ya kuruhusu ushindani, tofauti na miaka ya nyuma ya mashirika ya umma.

Ni wazi kuwa viwanda vitakwama kushindana kwenye dunia ya ushindani ya sayansi na teknolojia ndiyo maana vingine vimekuwa maghala ya kuhifadhia bidhaa toka nje.

Kwa mtizamo huo, ufumbuzi utapatikana kwa serikali kuweka mazingira ya kugharamia uzalishaji katika ugumu huo.

Katika kutimiza azma hiyo serikali inaweza kupunguza ugumu kwa kufikisha na kuvipa viwanda maji na nishati bure, lakini kujenga miundombinu reli na barabara kuvipa unafuu hata kama gharama ni kubwa.

Ikiwapa maji na nishati bure wenye viwanda watazalisha nyumbani na kupunguza uagizaji nje ili kuongeza ajira, kodi na kuchangia uchumi shindani wa viwanda.

Pamoja na kazi ngumu Ben Mkapa, ataendelea kukumbukwa na Tanzania siku zote kwa kuweka misingi ya kukuza uchumi imara, unaohusisha sekta binafsi, ya umma na sekta

Ndiye mwasisi wa taasisi imara za kusimamia mambo mengi kama TRA kodi, BRELA usajili wa biashara na leseni, NHIF Mfuko wa Bima ya Afya, HESLB kusimamia mikopo ya elimu ya juu na TANROADS kwenye barabara.

Kadhalika, ameboresha utumishi na ajira za umma, maslahi na kuweka nidhamu ya wafanyakazi wa serikali.





## Kanisa FAT kuwakemea viongozi wanaomhujumu Rais Samia

**Na Peter Mkwavila,** MANYONI

ASKOFU Mkuu Msaidizi wa Kanisa la Free Angalican of Tanzania, Daniel Makavu, amesema kuwa kanisa hilo litaendelea kuwakemea viongozi wanaomhujumu Rais Samia Suluhu Hassan, kukwamisha maendeleo ya nchi.

Pia, alisema Kanisa halitakaa kimya na kufumbia macho kwa viongozi wa namna hiyo ambao wamepewa dhamana na Rais ambao wanamwangusha badala ya kumsaidia ili maono yake yaweze kutimia kwa ajili ya Watanzania.

Askofu Mkavu alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waumini wa madhehebu mbalimbali kwenye ibada iliyofanyika katika Kanisa la Free la Angalican of Tanzania lililopo Kintinku wilaya ya Manyoni.

Makavu alisema kanisa hilo pia litaendelea kufanya maombi kwa ajili ya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa ili kuliepusha taifa kuwapata viongozi wabovu wasio waaminifu kwa wananchi.

Alisema hivi sasa serikali inahakikisha maendeleo yanawafikia watu wake kwa kufikisha huduma mbalimbali ikiwemo matibabu, elimu na barabara.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kintinku wilayani Manyoni, Maiko Maloda, aliwaomba viongozi wa dini kutumia nafasi zao kuwahimiza waumini kuomba na kufunga ili Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika uwe wa haki na amani.

Aidha, viongozi hao wa dini wametakiwa kukemea vitendo vinavyofanywa na jamii ikiwemo utoaji na upokeaji wa rushwa na mauaji dhidi ya watoto na watu wenye ulemavu.

Maloda alisema serikali inawategemea viongozi wa dini katika kusaidia nchi kuwa amani na utulivu.

Hata hivyo alisema bado jitihada za kukemea vitendo vinavyomchukiza Mungu inahitajika ikiwemo masuala ya ushoga na matumizi ya dawa za kulevya ambavyo vijana walio wengi wameathirika.

Alisema: "Haya yote serikali peke yake kuyakemea kamwe haiwezi bila msaada wa kutoka kwa viongozi wa dini kwa kushirikiana na waumini wake, hivyo niwaombe muendelee kuiombea serikali pamoja na watendaji wake".

# Barabara za zege milimani zamkosha Simbachawene

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameupongeza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuanza kujenga barabara za zege kwenye milima mikali iliyopo Kata ya Mang'aliza-Kibakwe wilayani Mpwapwa.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu inayosimamiwa na TARURA.

Ziara hiyo inafanywa na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia miundombinu, Rogauts Mativila.

"Niwashukuru sana TARURA na kuwapongeza kwa kutusaidia tulio kwenye mazingira magumu, jimbo langu la Kibakwe lipo katika maeneo tambarare na milimani na hii ni milima mikali ambayo ipo karibu kata sita na hakuna namna yoyote ya kutengeneza barabara zaidi ya barabara za zege" alisema.

Alisema utaratibu huo wa TARURA kujenga barabara za zege waliouanza miaka michache iliyopita umeanza kuleta ufanisi mkubwa hususani kufungua maendeleo pamoja na kuwaletea huduma nyingine wananchi ikiwemo umeme, shule pamoja na kituo cha afya.

"Kata ya Mang'aliza haikuwa na maendeleo kabisa lakini hii barabara ilivyofunguliwa hivi karibuni imeleta maendeleo kwa wananchi kwakuwa miaka ya nyuma nilikuwa nakuja huku kwa pikipiki lakini sasa hivi nakuja kwa gari na hata magari makubwa yanafika kuleta vifaa vya ujenzi ambapo kuna shule ya sekondari inajengwa, kwasababu sehemu korofi zote wameweka zege, kwakweli nawapongeza TARURA", alisema Simbachawene.

Aliongeza: "Hata hivyo ombi langu waendelee kutenga fedha kwa maeneo mengine kwani ilani na sera yetu sasa ni kuwapelekea umeme na huduma nyingine wananchi lakini changamoto ilikuwa ni barabara ila kusema ukweli TARURA wamejitahidi sana".

Aidha, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutafuta rasilimali fedha.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Rogatus Mativila, alisema mlima huo wenye urefu wa kilimota tano umekuwa mgumu kupitika wakati wote.

Alisema TARURA wametengeneza maeneo korofi kwa kujenga barabara za zege la saruji iliyochanganywa na kototo pamoja na nondo ili barabara hiyo ipitike ili kuwezesha shughuli za uzalishaji mkubwa unaoafanywa na wafugaji na wakulima wa mazao mbalimbali.

Mativila alisema Ofisi ya Rais -TAMISEMI wataendelea kuhakikisha mlima huo unaboreshwa na kupitika muda wote na kuendelea kutoa fedha zaidi ili wananchi waendelee kuzalisha mazao mbalimbali na kupatiwa huduma za kijamii ikiwemo shule na afya.



Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kintinku, wilaya ya Manyoni, mkoani Singida, Maiko Maloda, akizungumza na waumini wa madhehebu ya dini kwenye ibada ya kumpongeza Askofu Mkuu Msaidizi wa Kanisa la Free Anglican of Tanzania, Daniel Makavu, baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo, iliyofanyika katika Kanisa la Kintinku, Jumapili. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wanafunzi wazua taharuki bundi wakitua shuleni

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

TAHARUKI imezuka katika Kijiji cha New Kiomboi wilayani Iramba mkoani Singida baada ya ndege aina ya bundi watano kupatikana katika Shule ya Msingi Igumo.

Hatua hiyo ni siku chache tu baada ya wanafunzi wa shule hiyo kukumbwa na mapepo na kuanguka ovyo wanapokuwa shuleni hapo.

Mwalimu wa shule hiyo, Victoria Temba, aliwaeleza jana viongozi wa madhehebu ya dini mbalimbali wanaounda Kamati ya Amani Wilaya ya Iramba ambao walifika shuleni hapo kwa ajili ya kuwaombea wanafunzi waliokumbwa na mapepo.

"Wanafunzi wetu kwa takribani wiki tatu wamekuwa wakifika shuleni wanapagawa wakidai ndani ya darasa kwenye kona kuna nyoka na bibi ambaye anakuja darasani na kukaa nyuma kwenye kona na chooni, wanapokwenda kujisaidia kuna watu wanawapaka dawa ili wasifanye vizuri kitaaluma," alisema.

Temba alisema hali hiyo imesababisha wanafunzi katika shule hiyo kila mara kupata mapepo hususani wanapokwenda chooni hali iliyoathiri masomo darasani.

Kutokana na tatizo hilo viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali wakiongozwa na Askofu Yona Suleiman wa Kanisa la TAG KFC Kiomboi na Katibu wa UWT Wilaya ya Iramba, Judith Laizer walifika shuleni hapo kufanya maombi maalum kuiombea shule na wanafunzi hao.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida wanafunzi waliokuwa wakiombewa walikuwa wakitaja jina la bibi kizee mmoja (jina tunalihifadhi) ambaye walidai anawatumikisha mambo ya kishirikina shuleni hapo.

Pia, wakati maombezi yakiendelea mwanafunzi mmoja alipandisha mapepo, huku akisema bibi kizee huyo muda huo yupo kwenye dari la darasa la awali anachungulia jinsi maombi yanavyofanyika.

"Kuna mtu yupo kwenye darasa lile pale ninaomba mkamtoe na mkimkamata tu wanafunzi wote watakombolewa watakombolewa. Nendeni mkamkamate mtukomboe sisi tuwe huru," alisikika akisema mwanafunzi huyo.

Wakati maombi yakiendelea wanamaombi hao walifanikiwa kuwakamata bundi watano waliotoka madarasani na baadae kuwachoma moto mbele ya wananchi wa Kijiji cha Igumo.



## NFRA kununua tani 91,000 za mahindi, mpunga

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Makambako mkoani Njombe imejipanga kununua tani 91,000 za mahindi na mpunga kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Kati ya tani hizo, mahindi ni tani 66,000 na mpunga ni tani 25,000.

Hayo yalibanishwa jana na Meneja wa NFRA, Kanda ya Makambako, Revocatus Bisama wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema NFRA unanunua mahindi kilo moja kwa shilingi 650 kwa kituo cha Makambako na kituo cha Igula Ilembula kilichopo wilayani Wanging'ombe ni shilingi 600 kwa kilo moja, huku mpunga ikinunua kwa kilo moja kwa shilingi 750 kwa vituo vilivyopo vijijini na mjini Makambako ni Sh. 800.

Alisema kuwa wakala huo umeaanza kununua mahindi na mpunga kwenye baadhi ya wilaya hasa Wanging'ombe na Mbarali.

Alisema wakala utaendelea kufungua vituo vingine vya kununulia mahindi ikiwemo kituo cha Igwachanya wilayani Wanging'ombe na vituo vingine vinne katika Wilaya ya Ludewa na Mkoa wa Iringa katika maeneo ya Ilula, Isimani na Pawaga, huku Mbarali ikiwa ni eneo la Madibila na Uturo.

Hata hivyo alisema kila mkulima anaruhusiwa kupeleka mahindi katika vituo vyote vimefunguliwa, huku akiwawataka kuzingatia ubora wa mahindi na mpunga wanaotaka kuuza.

"Tumejiwekea malengo kwa mwaka 2024 hadi 2025 lengo la ununuzi wa mpunga ni tani 25,000 na lengo la kununua mahindi tani 66,000 kwa hiyo jumla tunategemea kununua tani 91,000," alisema Bisama.

Baadhi ya wakulima kutoka Makambako akiwemo Veronica Mtitu alisema bei hiyo ambayo imewekwa na serikali siyo rafiki kwa sababu ya ukubwa wa gharama ambazo zimetumika wakati wa kilimo.

# Njombe yapokea bil.9.2/- ujenzi shule za sekondari

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MKOA wa Njombe umepokea Sh. bilioni 9.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari na kufanya maboresho katika sekta ya elimu.

Hayo yalielezwa na Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Farida Mwasumilwe wakati akitoa taarifa katika kikao cha uwasilishwaji wa fedha za miradi mwaka mpya wa fedha 2024/25.

Mwasumilwe alisema kila halmashauri imepokea kiasi chake ambapo Ludewa imepokea shilingi bilioni 1.9, Makambako Sh.milioni 604, Makete Sh. milioni 2.8, Njombe wilaya milioni Sh. 911.3, Njombe Mji Sh.milioni 636 na Wanging'ombe Sh. bilioni 2.3.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe Anthony Mtaka alisema mwaka wa fedha ulipoanza tayari Mkoa wa Njombe umepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya.

"Mchanganuo huo usemwe hapa ili kila mtu kwenye halmashauri yake ajue amepokea kiasi gani kwa ajili ya kujenga madarasa mangapi, eneo hili kujenga vyoo na eneo hili kujenga bweni, ili pia kupata uelewa wa pamoja," alisema Mtaka.

Mtaka alisema lengo la kikao hicho pia ni kusaidia kuweka mikakati ya kuanza kwa ujenzi kwa pamoja ili kuweza kukamilisha kwa wakati.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari alisema wakurugenzi wanapaswa kujipanga namna ya kwenda kutekeleza ujenzi mapema ili ifikapo Januari mwaka 2025 watoto waweze kuingia kwenye shule mpya.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga alisema kwa awamu ya kwanza serikali imetoa Sh. bilioni 9.2 siyo kitu kidogo ni fedha nyingi hivyo zinapaswa kusimamiwa vizuri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli alisema wamejipanga kuhakikisha wanasimamia vizuri ujenzi huo ili kuleta tija kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe alisema katika halmashauri hiyo watoto 549 kati yao 548 wa kidato cha sita wamepata kati ya daraja la kwanza na la tatu na mmoja pekee akipata daraja la nne, huku sababu akitaja kuwa ni kutokana na uboreshaji wa miundombinu katika sekta hiyo.

Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya elimu mkoani Njombe umeonekana kuleta mafanikio kitaaluma ambapo matokeo ya kidato cha sita kitaifa mwaka huu mkoa umepanda kutoka asilimia 96.86 hadi asilimia 100.



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kusini, Grayson Shilongoji, baada ya kuendesha harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa kanisa la Ihami, Usharika wa Ikwete, Jimbo la Makambako, mkoani Njombe juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara afariki dunia baada ya kuvamiwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MFANYABIASHARA katika Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, Godfrey Ndambo (45) amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu baada ya kuvamiwa nje ya geti nyumbani kwake na majambazi.

Majambazi hao walimpiga na kitu kizito kichwani na kisha kumpora shilingi milioni 47.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 20 mwaka huu majira ya saa 2:30 usiku katika eneo la Uzunguni Kata ya Ramadhani Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Alisema wahusika wa tukio hilo ambao idadi yao haijafahamika walimpiga marehemu na kutoweka na fedha ambazo zinakadiriwa kuwa ni shilingi milioni 47 kulingana na taarifa kutoka kwenye biashara yake iliyofungwa siku hiyo kabla ya tukio.

"Baada ya kujeruhiwa alitibiwa katika Hospitali ya Kibena na baadaye alihamishiwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mbeya wakati matibabu yakiendelea akawa amefariki," alisema Banga.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi wa kina na punde watatoa taarifa ya watu watakaoshikiliwa kuhusika na tukio hilo.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara mkoani hapa kufunga kamera maeneo wanayoishi na ziwe wazi muda wote kwani linapotokea tukio ni rahisi kwa Jeshi la Polisi kuanza kufanya uchunguzi kupitia kamera hizo.

"Tatizo tulilopata pale kwa marehemu kuna CCTV kamera lakini haikuwa inafanya kazi kwahiyo mara nyingi alipokuwa anarudi nyumbani ndiyo alikuwa anaiwasha na kufanya kazi," aliongeza Banga.

Alisema wafanyabiashara wenye mitaji mikubwa wanapaswa kuhakikisha hawahifadhi fedha nyingi nyumbani kwani kwasasa zipo taasisi za fedha ambazo kupitia mashine zake wanaweza kuweka fedha zao hata nyakati za usiku.

Mwenyekiti wa Mawakala Mkoa wa Njombe, Erasto Mbembati alisema kutokana na matukio hayo kutokea na kusababisha vifo kwa wakala na wengine kujeruhiwa wamekubaliana kumuomba Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kikao ili kutafakari kwa pamoja sababu za tatizo hilo.

Alisema: "Kwa sababu inapoelekea hii biashara inaenda kuwa hatari hii ni biashara ambayo inavutia kwa majambazi, hatusemi kama Jeshi la Polisi halifanyi kazi lakini uwenda kuna tatizo mahali na tukikaa pamoja sisi na wao tunaweza tukasaidiana"



# Watu 17 wafariki dunia ajali za barabarani Juni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU 17 wamefariki dunia kwenye ajali 23 zilizotokea kipindi cha Juni 2024, mwendokasi na uzembe wa madereva umetajwa kuwa chanzo cha ajali hizo.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Asha Mussa Mahfoudh, akiwasilisha ripoti ya takwimu za ajali na makosa ya barabarani jana visiwani hapa alisema idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 15.0 kutoka ajali 20 zilizoripotiwa Mei 2024.

Aidha, alisema idadi ya waliofariki nayo imeongezeka kwa asilimia 21.4 kutoka waathirika 14 waliofariki Mei 2024, huku Wilaya ya Kati ikiongoza kwa ajali nne sawa na asilimia 17.4 ikilinganishwa na wilaya nyingine.

Alisema kati ya ajali 20 zilizoripotiwa, ajali 15 zilisababishwa na kuendesha gari kwa mwendokasi na ajali nane zilisababishwa na uzembe wa dereva.

Aliitaja Mikoa ya Kusini Unguja na Kaskazini Pemba ndiyo iliyoongoza kwa kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendokasi.

Aidha, alisema jumla ya makosa 3,599 yaliripotiwa Juni 2024 ambapo makosa 3,592 yalifanywa na wanaume na saba yaliripotiwa kwa wanawake.

Alilitaja kosa kuu lililoripotiwa ilikuwa ni kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (1,811), yakifuatia na kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (492) na kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 384).

Baadhi ya wananchi visiwani Zanzibar, walisema bado jitihada zinahitajika katika kuhakikisha madereva wanafuata sheria za barabarani ili kupunguza ajali.

Khamis Ali ni miongoni mwa wananchi hao, alilitaka Jeshi la Polisi kuendelea kupambana katika kupunguza ajali barabarani kwa kufanya operesheni mbalimbali kwa kushirikiana na mamlaka nyingine.



Baadhi ya wananchi wakiangalia wanyama aina ya kobe, walipotembelea kisiwa cha Prison, kilichoko katika Bahari ya Hindi, nje kidogo ya mji wa Malindi Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watendaji serikali watakiwa kuwa wabunifu, waaminifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar (mawasiliano), Dk. Mzee Suleiman Mndewa amewataka watendaji waliopewa dhamana ya kuratibu masuala ya TEHAMA katika taasisi za serikali kuwa wabunifu na waaminifu wakati wakitekeleza majukumu yao.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya mfumo wa anuani za makazi, majaribio ya utoaji wa barua za utambulisho wa makazi yaliyowashirikisha waratibu wa mfumo wa anuani za makazi.

Kikao hicho kilifanyika katika ukumbi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA).

Alisema kazi za serikali zinahitaji ubunifu utakaosaidia kuleta tija kwa serikali na jamii kwa ujumla jambo ambalo kwa namna moja au nyingine litasaidia kurahisisha kazi, muda na kuweka umakini katika utendaji.

Aidha, alisema mfumo huo unalenga kwenda kurahisisha kazi za masheha kuwa katika njia ya kidijitali ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia.

Mratibu msaidizi wa mfumo wa anuani za makazi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Tanzania Bara, Mkude Arnold alisema lengo la serikali katika uwekezaji wa mfumo huo ni kuwezesha serikali katika utoaji na ufikishaji huduma kwa wananchi kupitia mfumo wa anuani za makazi.

Mkude alisema mfumo huo wa utoaji wa huduma unakwenda kumuondolea mwananchi changamoto ya upatikanaji wa huduma zinazotolewa na viongozi wa shehia.

Alisema huduma hiyo ya kutumia mfumo wa utoaji wa barua kidijitali tayari umeshazinduliwa kwa upande wa bara, hivyo Julai 24 mfumo huo utazinduliwa kwa upande wa Zanzibar.

Mratibu kutoka Idara ya Mawasiliano Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Issa Hamad alisema kuwa, mfumo ulioanzishwa umeanza kutoa tija katika matumizi mbalimbali ambapo katika sekta ya utalii utawawezesha watembeza watalii na wageni kutambua sehemu mahsusi wanazohitaji kufika bila ya kuuliza.

Mratibu wa anuani za makaazi kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Rashid Mwinyi aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa makarani wanaopita katika maeneo yao kwa ajili ya kuhakiki taarifa zinazohusiana na anuani za makazi.

# Uharibifu mita za maji waisababishia hasara serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATUKIO ya uharibifu wa miundombinu ya kusambaza maji pamoja na mita za kusoma kiwango cha matumizi ya maji, kinaisababishia hasara serikali.

Hasara hiyo inatokana na serikali kutumia gharama kubwa kuhudumia miundombinu hiyo.

Matukio hayo yanayofanywa na baadhi ya wananchi kumeifanya bodi ya Mamlaka ya Maji safi na Salama Zanzibar (ZAWA) kufanya ziara ya kukagua miundombini hiyo iliyohujumiwa.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya ZAWA, Mohamed Aboud Mohamed, akiwa katika ziara hiyo juzi, alisema mikakati ya serikali ni kuhakikisha tatizo la uhaba wa maji linapatiwa ufumbuzi, kwamba juhudi mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo kutekeleza miradi ambayo inatokana na fedha za wafadhili pamoja na serikali yenyewe.

Alisema mradi wa uwekaji mita za kusoma matumizi ya maji unatekelezwa na Benki ya Exim kutoka India ambao unafanyika katika maeneo ya Kwarara, Bweleo hadi Fumba, huku lengo ni kuona matumizi halisi ya maji yanayofanyika kutoka kwa wateja.

Alisema uharibifu huo kwa kiasi kikubwa unarudisha nyuma juhudi za ZAWA katika kutoa huduma za uhakika kwa wateja na kupunguza usumbufu uliopo sasa wa kutoa bili kwa makisio.

"Matukio ya uharibifu yanayofanyika kwa kung'olewa miundombinu ya usambazaji wa maji safi na salama hayakubaliki hata kidogo na huko ni kurudisha nyuma juhudi za mamlaka katika usambazaji wa huduma hiyo kwa kiwango cha ubora kwa wananchi" alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Salama, Dk. Salha Mohamed Kassim alisema kitendo cha kung'olewa miundombinu ya usambazaji wa maji kwa wananchi kinarudisha nyuma juhudi za mamlaka kutekeleza malengo yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema malengo ya ZAWA ifikapo mwaka 2030 ni kuona huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 90 zinawafikia wananchi wa mjini na vijijini na ndiyo maana kazi kubwa ya kufikisha miundombinu ya huduma hiyo inavyotekelezwa na Serikali ya Zanzibar.

"Uongozi wa ZAWA umesikitishwa na matukio ya hujuma zinazofanywa na wananchi ambazo hazikubaliki kwani huko ni kurudisha nyuma juhudi za serikali na kuitia hasara" alisema.

Viongozi kutoka maeneo ya Kwaraka pamoja na Bweleo wamesikitishwa na matukio ya hujuma yanayofanywa na wananchi na kuwataka wazazi kukemea vitendo hivyo.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza mradi mkubwa wa kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji mjini na vijijini chini ya ufadhili wa Benki ya Exim kutoka India sambamba na kuweka mita za kusoma matumizi ya kiwango cha maji kwa wateja.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA CHARLES MAGAMBO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4063/0021** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CHIEF WANZAGI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/149361/2024**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**PAULINE PLASDUS MBITA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0139/0581** kilichotolewa na **MTWARA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/151582/2024.**

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**LUKA ANYIMILE MWAKANOSYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1492-0077** kilichotolewa na KYEJO SEKONDARI mwaka 2011. Cheti cha Chuo chenye namba **02/CBA-111/CJ/21D/006** kilichotolewa na **VETA CHANG'OMBE DAR ES SALAAM** mwaka 2022. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/72918/2024.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ANDREW PIUS MPONDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo (SHAHADA) chenye namba **BCOM002001** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/136286/2024.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**BRUNO EMROD MOSSI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2421/0039** kilichotolewa na **STARHIGH SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/151532/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GASTON MELTUS FRANCIS** naomba kutangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE160235** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu tarehe 06/08/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/143813/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUSUFU RAMADHANI NKUSA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Bedford yenye namba za usajili **T593ALK,** Model **TJ1090,** CHASIS NAMBA **701483,** ENGINE NAMBA **6572188.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/KON/30507/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ZUBERI HAMISI NGODA** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 725 DFU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/10779/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MAKERA INVESTMENT COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 531 BXG** aina ya **SANLG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/5512/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DANIEL JOHN KAROLI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 598 CYA** aina ya **SANLG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/5246/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHARLES MASHIMI MKONGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 642 CQF** aina ya **SANLG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/5234/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YONAH KISUDA NGOMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 843 DPZ** aina ya **SINORY** yenye jina la **TANZANIA CHINA TRADE, TOURISM DEVELOPMENT LTD.** Chassis namba **LD3PCJ6J0NZ001880.** Engine namba **SR156FMI22011880.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SIN/MAN/5363/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YOTHAM SHIGEMO MACKENZIE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 946 DNA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/24846/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **JESTINA JUMA**, mtu mzima mwenye akili timamu mkazi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatanvy:-

1. Kwamba, Mimi **JESTINA JUMA** ni msismamizi wa mirathi ya marehemu **JUMA JULIUS YOHANA.**
2. Kwamba, sikuwahi kujua kuwa marehemu aliacha mtoto anayeitwa **JAMES JUMA.**
3. Kwamba, hata hivyo familia itafurahi ikithibitika kwamba marehemu aliacha mtoto aitwaye JAMES JUMA kwani sisi kama familia hatukulitambua kuwa marehemu aliacha mtoto.

**UTHIBITISHO**

Mimi **JESTINA JUMA** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act. Cap. 34 R; E 2019).

**Imethibitishwa hapa Tanga**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

Sahihi ya Muapaji

**KUITWA SHAURINI**

**KWA VESTINA MAGNUS HILLY**

**MKAZI WA KIJIJI CHA MAPERA.**

Unaamuriwa kuja kuhudhuria mbele ya Baraza tukufu la kata ya Mapera ili kujibu lalamiko la Agustino Teodari Ndunguru kuwa umeingilia kwenye Shamba lake la Kahawa kukatia na kupiga dawa bila ridhaa yake kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hapo tarehe 30-07-2024 siku ya Jumanne saa 3:00 asubuhi bila kukosa. Kutokufika kwako ni kuvunja sheria ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania na utochukuliwa hatua kali za kisheria dhidi yako.

Sahihi **yako.....**

17-07-2024

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wabunge upinzani wakamatwa Uganda

**KAMPALA,** Uganda

WABUNGE watatu wa upinzani nchini Uganda wamewekwa kizuizini tangu Jumatatu kabla ya kesi yao kusikilizwa, huku polisi wakieleza kuwa viongozi hao walikamatwa katika mkesha wa maandamano dhidi ya ufisadi uliyopigwa marufuku.

Kwa mujibu wa kiongozi mkuu wa upinzani nchini humo, Bobi Wine, wabunge hao watatu waliokamatwa ni sehemu ya Jukwaa la Umoja wa Kitaifa (NUP), ambalo majengo yake yalizingirwa na polisi na wanajeshi waliokuwa na silaha.

**Waganda wanapokwenda bungeni kuandamana, wanapaswa kufahamu kuwa serikali iko tayari kumwaga damu yao ili kusalia madarakani.**

Msemaji wa Polisi Uganda, Kituuma Ruspke alisema jana kwamba kupelekwa maofisa hao wa polisi kuliamuliwa kwa sababu za kiusalama. Na kwamba kulikuwa na habari za kuaminika kwamba umati mkubwa ungehamasishwa kuhudhuria mkutano wa waandishi wa habari uliopangwa Julai 22, mwaka huu na upinzani.

Ruspke alisema wabunge hao watatu na watu wengine saba walifikishwa mahakamani jana, na kushtakiwa kwa makosa mbalimbali na kuwekwa jela.

Aidha, ilielezwa kuwa hakutoa maelezo zaidi kuhusu mashtaka yao lakini msemaji wa NUP, Joel Ssenyonyi alisema wabunge hao walishtakiwa kwa kukiuka sheria za barabarani na kuwazuia maofisa wa polisi, mashtaka ambayo wanayakanusha.

Wabunge hao ni Francis Zaake, Charles Tebandeke na Hassan Kirumira, wote wa chama cha upinzani cha NUP na kwamba watafikishwa mahakamani kesho kwa ajili ya kusikilizwa shauri lao la kuachiwa kwa dhamana.

Hata hivyo, upinzani umeapa kuendelea na maandamano ya kupinga ufisadi licha ya kupigwa marufuku na polisi. "Tutaandamana kesho chochote kitakachotokea," alijibu, Shamin Nambasa, mmoja wa waandamanaji aliyehojiwa na shirika la habari la AFP.

"Waganda wanapokwenda bungeni kuandamana, wanapaswa kufahamu kuwa serikali iko tayari kumwaga damu yao ili kusalia madarakani, lakini hilo lisiogopeshe mtu yeyote," alisema mpinzani Bobi Wine, ambaye jina lake halisi ni Robert Kyagulanyi.

Rais Yoweri Museveni, ambaye ameiongoza nchi hiyo kwa karibu miongo minne, alionya kuwa Waganda wanaopanga kuandamana mitaani wanacheza na moto. **RFI**

## Vijana waonywa kuandamana uwanja ndege

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la Polisi nchini Kenya limewaonya waandamanaji kuepuka kuandamana kuelekea Uwanja wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta na maeneo yaliyo karibu na uwanja huo, baada ya Gen Z kudai kuwa wataenda kukusanyika katika maeneo hayo.

Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ya Kenya jana iliwashauri abiria wanaotumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta kufika mapema kuliko kawaida. Tahadhari hiyo inatokana na hatua ya baadhi ya waandamanaji kujipanga kukusanyika katika maeneo ya uwanja huo.

Kaimu Inspekta Jenerali wa polisi nchini humo, Douglas Kirocho aliwaonya waandamanaji dhidi ya jaribio hilo la kuuvamia uwanja wa ndege akisema polisi ina ripoti za kijasusi zinazoonyesha maandamano ya sasa yametekwa nyara na wahalifu.

Katika siku chache zilizopita polisi ilisema maandamano, ambayo yamegharimu maisha ya watu karibu 50 tangu kuanzishwa kwake mwezi mmoja uliopita yameingiliwa na magenge ya wahalifu.

Hata hivyo, Rais wa Kenya William Ruto alisema maandamano hayo lazima yakomeshwe, huku upinzani wakihimiza haki, wakieleza kuwa vijana hao wataandamana hadi kiongozi wa taifa hilo atakapoondoka madarakani.

Ilielezwa kuwa vijana wamekuwa wakiongoza maandamano nchini Kenya wakipinga hatua ya serikali kuongeza ushuru, licha ya Rais Ruto kuondoa muswada wa fedha wa 2024/2025 na kulifuta karibu baraza lake lote la mawaziri, na kwamba baada ya kulifanyia marekebisho aliwarejesha kazini baadhi ya mawaziri katika baraza hilo wiki iliyopita.

Wachambuzi wa siasa walisema vijana hao wanataka mageuzi katika kupambana na ufisadi, utawala bora na utoaji wa huduma zilizobora zaidi katika serikali za kaunti na kuu. **DW**



Makamu wa Rais wa Marekani aanza kampeni baada ya kuteuliwa kushiriki katika kinyang'anyiro cha kugombea kiti cha urais katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# Kamala: Nina uhakika kumshinda Trump

**NEW YORK,** Marekani

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris ambaye amezindua kampeni za kutafuta uungwaji mkono kutoka kwa wajumbe wa chama chake, amesema ana uhakika wa kumshinda mgombea wa Chama cha Republican, Donald Trump, aliyemwelezea kama mtu asiyekuwa na sifa za kuongoza kutokana na kesi mbalimbali zinazomwandama.

Aidha, ilielezwa kuwa hadi jana amepokea michango ya dola milioni 81 sawa na Sh. bilioni 217.89 ndani ya saa 24 za kwanza tangu Rais wa taifa hilo, Joe Biden kumteua kugombea katika kinyang'anyiro cha urais katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Ilibainishwa kuwa kampeni hiyo imepokea zaidi ya michango 888,000 kutoka kwa wafadhili ambao asilimia 60 wamechangia kwa mara ya kwanza wakati wa mzunguko wa uchaguzi wa mwaka huu.

Pia kamati kubwa ya kisiasa ya kidemokrasia nchini humo ilibainisha kwamba imepokea dola milioni 150 zaidi ya Sh. bilioni 400, katika ahadi mpya kutoka kwa wafadhili wakuu ndani ya saa 24 zilizopita.

Mashirika ya habari ya associated Press na Reuters, yalisema mwanamke huyo wa kwanza mweusi kuwania nafasi hiyo nchini Marekani, amepata uungwaji mkono unaotakiwa kutoka kwa wajumbe wa chama chake cha Democratic ili kupata tiketi ya kuwania urais.

Aidha, ilibainishwa kuwa hadi sasa Kamala amefanikiwa kupata uungwaji mkono kutoka majimbo 20, yanayofikisha jumla ya wajumbe 2,538 na kupitia idadi ya wajumbe 1,976 wanaotakiwa ili kupata tiketi ya Chama cha Democratic.

Kadhalika, shirika la habari la Reuters liliripoti likinukuu vyanzo mbalimbali kwamba wenyeviti wote wa majimbo 50 nchini Marekani wa chama hicho watamuunga mkono Kamala.

Vile vile, wajumbe wa chama hicho wanatarajiwa kuthibitisha hatua hiyo wakati wa mkutano mkuu Agosti 7, mwaka huu watakapokutana jijini Chichago iwapo hawatobadilisha uamuzi wao.

Katika hatua nyingine, Spika wa zamani Nancy Pelosi ametanagaza kumuunga mkono Kamala huku kauli za vigogo wengine wa chama hicho kama kiongozi wa Chama cha Democratic kwenye Senate, Chuck Schumer ikisubiriwa.

Bill Clinton, Rais wa zamani wa Marekani pamoja na mkewe Hillary, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya kigeni chini ya Rais Barrack Obama, wamekwishatangaza kumuunga mkono Kamala Harris.

Majina mengine makubwa kuanzia kiongozi wa wengi katika Baraza la Seneti Chuck Schumer na Rais wa zamani Barack Obama, wamejaribu kujizuia kusema lolote kuhusiana na hatua hiyo ya kumwidhinisha Kamala, ingawa walimpongeza Biden kwa kujiengua.

Taarifa ya Obama ilisema kwamba watafuatilia mwenendo katika siku zijazo, na kuongeza kuwa ana imani kubwa kwamba viongozi wa chama chake cha Democratic wataweza kuanzisha mchakato utakaoibua mgombea imara. **RFI/DW**

HABARI MICHEZO

# APR KUITUMIA MECHI NA SIMBA MAANDALIZI KUIVAA AZAM CAF

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya APR ya Rwanda, limesema mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Simba watakaoucheza Agosti 3, mwaka huu, katika kilele cha kuadhimisha ' Siku ya Simba maarufu Simba Day, utawasaidia kuwapima wachezaji wao kuelekea kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika dhidi ya Azam FC.

APR itakutana na Azam FC katikati ya mwezi ujao kwenye mechi ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mshindi wa jumla atakutana na timu itakayopata matokeo ya jumla kati ya JKU ya Zanzibar na Pyramids ya Misri.

Akizungumza na Nipashe mapema wiki hii jijini Dar es Salaam, Kocha wa timu hiyo, Thierry Hitimana, alisema mchezo huo ni kipimo tosha kwa kuwa wanakutana na Simba ambayo pia inajiandaa na mashindano ya kimataifa.

"Mchezo huo ni kipimo kwa wachezaji wangu kwani tutacheza na timu ambayo inajiandaa na mashindano ya kimataifa, vilevile utazidi kuimarisha viwango vyetu," alisema Hitimana.

**Katika hatua nyingine, alisema mchezo wao dhidi ya Azam FC, utakuwa na upinzani mkubwa na kudai anawafahamu wapinzani wao hao vizuri.**

"Azam ni timu nzuri, tumeona aina ya usajili wao pamoja na kushika nafasi ya pili msimu ujao, tutapambana kuhakikisha tunaanza vizuri," alisema.

Aidha, alisema baada ya kumalizika kwa mashindano ya Dar Port Cecafa Kagame Cup 2024 wiki iliyopita, waliendelea kubaki Dar es Salaam wakiendelea na maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Simba.

Aliongeza kuwa anafurahishwa na ushirikiano unaofanywa na mashabiki wa soka hapa nchini kwa kuzipa hamasa timu za nje licha ya kuwa timu za Tanzania zilitolewa mapema.

## HIZI HAPA...




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evance Mtambi, akionyesha moja ya jezi zitakazotumika katika mbio za Serengeti Migration Marathon na Antipoaching Run jana, zinazotarajia kuanza Agosti 3, mwaka huu mjini Mugumu na Fort Ikoma wilayani Serengeti. **MPIGAPICHA WETU**

# *Serikali yawataka wasanii kurejesha mikopo*

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imewataka wasanii waliochukua mikopo kwenye Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, kuirejesha ili iweze kuwasaidia wengine.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, wakati alipokuwa anazungumza na viongozi wa mashirikisho mbalimbali ya sanaa nchini.

"Kwa wale wasanii ambao wamechukua mikopo kwenye huu mfuko wanapaswa kurudisha kama makubaliano yalivyokuwa ili ziweze kusaidia wasanii wengine wenye wanaohitaji," alisema Mwinjuma.

Aidha, alimtaka Mtendaji Mkuu wa mfuko huo akae upya na wale ambao hawajaanza kurudisha fedha hizo ili awaelekeze jinsi zinavyotakiwa kulipwa.

Alisema baada ya kuona wasanii hao wamekuwa wagumu kulipa wapo kwenye mchakato wa kuwalegezea masharti ili kila mmoja aweze kuzirudisha.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Nyakaho Mahemba, alisema anamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuuongezea fedha mfuko huo ambao lengo ni kunufaisha wasanii ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kutuongezea bilioni tatu katika mfuko wetu ambazo zitamnufaisha kila msanii aweze kutimiza malengo yake, hivyo kila aliyechukua anapaswa kurudisha," alisema Mahemba.

Wakati huo huo, Rais wa Shirikisho la Sanaa ya Muziki Tanzania, Ado Novemba, alisema anaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaongezea fedha hizo ambazo zimewanufaisha kwa kiasi kikubwa.

"Tunaahidi kulipa fedha hizo kwa wale ambao wameshindwa kulipa naamini watabadilika na kulipa ili kumuunga mkono rais wetu," alisema Novemba.

Jacob Stephen maarufu JB, ambaye ni msanii wa filamu aliyewawakilisha wasanii wenzake, alisema watakutana na wasanii wenzake wajadiliane jinsi ya kurejesha fedha hizo kwani hawataki kumuangusha rais.

"Tunaahidi kulipa madeni hayo, hatutakubali kujitia aibu kwa mama yetu Samia kwa kushindwa kulipa fedha ambazo zinatunufaisha sisi wenyewe," alisema JB.

# KMC kukipiga na timu ya Marekani

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KMC inatarajia kujipima nguvu na PCC Eagles Men's Soccer ya Marekani, katika mchezo wa kirafiki unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, jana alisema kuwa lengo la mchezo huo pamoja na kukuza mahusiano, lakini pia kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunacheza na timu hiyo kutoka Marekani na pambano hilo limeandaliwa na Kanisa la Faith Baptist, tutacheza Uwanja wa Jamhuri, Morogoro na hautakuwa na kiingilio," alisema Ofisa Habari huyo.

PCC Eagles Men's Soccer ambayo maskani yake ni Pensacola, Florida, Marekani, inamilikiwa na Chuo cha Michezo cha Taasisi moja ya Kidini nchini humo.

KMC tayari imeshaanza maandalizi ya msimu ujao ikiwa imefanya usajili wa wachezaji wapya ambao wanaona watawasaidia msimu ujao, chini ya kocha raia wa Somalia, Abdihamid Moallin.

Wachezaji waliowasajili wa KMC kwa ajili ya msimu ujao ni kipa, Imasil Mpaki kutoka Biashara United, Ajoh Austin, straika kutoka Cameroon, Oscar Paul, kiungo mshambuliaji Mtanzania aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Kenya katika Klabu ya Kakamega Home Boys, beki wa kati, Nickson Kassam Mosha, akitokea kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar.

Wengine ni kipa raia wa Burundi aliyekuwa akiidakia Klabu ya Vipers ya Uganda, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana kutoka Vital'O ya Burundi na beki wa kati Salum Athumani 'Stopper' kutoka KVZ ya Zanzibar.



## ZISIKUPITE

### EZE ATAKIWA CITY

MANCHESTER City inatafuta kumnunua winga wa Crystal Palace, Eberechi Eze, 26, huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa England akiwa na kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 60 pamoja na nyongeza. ***(Mirror)***

### BRUYNE ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Ittihad, inamtaka mchezaji wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, 33, jambo ambalo limesababisha Manchester City kufikiria kumnunua Eberechi Eze. ***(Guardian)***

### DONNARUMMA AIVUTIA CITY

MANCHESTER City inavutiwa na mlinda mlango wa Paris St-Germain na Italia, Gianluigi Donnarumma, 25, huku wakitafuta kuchukua nafasi ya Ederson, kipa mwenye umri wa miaka 30 wa Brazil, ambaye anaweza kuhamia Al-Ittihad. ***(Sky Sports Italia)***

### EDERSON KUACHIWA CITY

GOLIKIPA Ederson atagharimu angalau pauni milioni 40 ikiwa Al-Ittihad inataka kumsajili kutoka Manchester City, ambao wako tayari kumwacha kipa huyo aondoke mradi tu hesabu yao iafikiwe. ***(ESPN)***

### SPURS KUMUUZA RICHARLISON

KLABU ya Tottenham Hotspur inamthaminisha mshambuliaji wa Brazil, Richarlison, 27, kwa pauni milioni 60, huku Klabu ya Saudi Arabia ya Al-Ahli ikionesha nia kumtaka mchezaji huyo. ***(Times)***

### NKETIAH, GUEHI KUPISHANA

KLABU ya Arsenal iko tayari kumtoa mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25, kama sehemu ya makubaliano ya kubadilishana na Crystal Palace kumnunua beki wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24. ***(Metro),***

### SANCHO AWANIWA PSG

KLABU ya PSG inamtaka winga wa Manchester United, Jadon Sancho, 24, na mchezaji huyo wa Kimataifa wa England anaonekana kuwa tayari kwa wazo la kujiunga na mabingwa hao wa Ufaransa. ***(foot Mercato)***

### BRUNO NAYE AWINDWA

KLABU ya PSG itajaribu kufanya makubaliano na Manchester United kumnunua Jadon Sancho, lakini pia wanamtaka kiungo wa kati wa klabu hiyo ya Old Trafford na Ureno, Bruno Fernandes, 29. ***(L'Equipe - In French)***

### FELIX ASAKWA VILLA

ASTON Villa inalenga kumnunua fowadi wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix, 24, baada ya kukubali kuuzwa kwa winga Mfaransa Moussa Diaby, 25. ***(Guardian)***

### GIL, REGUILON WAACHWA

WINGA wa Tottenham Hotspur, Bryan Gil, 23 na beki wa kushoto, Sergio Reguilon, 27, ambao wote ni Wahispania, wameachwa katika ziara ya kujiandaa na msimu mpya wa klabu hiyo Japan na Korea Kusini ili waweze kutafuta uhamisho kutoka kwa klabu hiyo. ***(Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE KUIKOSA SPURS

**LONDON,** England

HARRY Kane atakosa mechi ya Bayern Munich ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur mjini Seoul, kocha Vincent Kompany amethibitisha Jumatatu.

**Nahodha huyo wa England alihamia Bayern majira ya joto yaliyopita kwa mkataba wa thamani ya Euro milioni 120 na alimaliza msimu akiwa mfungaji bora wa Bundesliga baada ya kupachika mabao 36.**

Licha ya uchezaji wake, Bayern ilimaliza katika nafasi ya tatu kwenye jedwali, pointi 18 nyuma ya mabingwa Bayer Leverkusen.

## ●●● Yumo pia Davies, Upamecano na Coman, lakini watakuwapo kwenye mechi...

Kane alipata jeraha la mgongo msimu huu wa Euro, huku akiifungia England mabao matatu walipofika, lakini walipofika fainali alikosa makali mbele ya lango.

Bayern watasafiri hadi Korea Kusini kama sehemu ya maandalizi yao ya msimu ujao, ambapo wanatazamiwa kumenyana na Tottenham Hotspur Agosti 3, mwaka huu.

"Harry Kane, Alphonso Davies, Dayot Upamecano na Kingsley Coman hawatakuwapo, lakini tunatumai watakuwapo kwenye mechi ya kwanza ya ligi," alisema kocha mpya wa Bayern, Kompany katika mkutano wake na waandishi wa habari.

Hata hivyo, Kane atakuwa na fursa nyingine ya kumenyana na timu yake ya zamani wakati Bayern watakapocheza na timu hiyo ya London Kaskazini kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur Agosti 10, mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, aliondoka Tottenham akiwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo akiwa na mabao 280 kwa jumla.

Msimu wa Bayern utaanza dhidi ya SSV Ulm Agosti 16, mwaka huu katika raundi ya kwanza ya Kombe la DFB.

# YORO: FERDINAND KANISHAWISHI KUTUA KWANGU MAN UNITED




**LOS ANGELES,** Marekani

LENY Yoro amekiri kwamba gwiji wa Manchester United, Rio Ferdinand, alichangia kwa kiasi kikubwa kumshawishi kuhamia Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alijitokeza kwa mara ya kwanza akiwa amevalia jezi ya United Jumamosi, wakati waliposhinda mabao 2-0 dhidi ya Rangers katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya, baada ya kukataa nafasi ya kusubiri mwaka mmoja ili kujiunga na Real Madrid.

Sasa, katika mahojiano yake ya kwanza tangu ahamie Old Trafford, Yoro amefichua mazungumzo aliyofanya na Ferdinand - ambaye mwaka 2002 alikuwa mwanasoka ghali zaidi wa Uingereza katika historia wakati huo alipojiunga na United na beki wa pili ghali zaidi duniani.

"Ilikuwa kama wiki mbili zilizopita nilipozungumza na Rio kwa mara ya kwanza," alisema Yoro akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Alinipigia simu. Kwanza kabisa, nilifurahishwa sana kuzungumza naye na ndio, tulizungumza kama dakika 10 kuhusu Man Utd.

"Alinisaidia sana kufanya chaguo langu. Ilikuwa heshima sana kuzungumza naye. Alizungumza nami kuhusu klabu, na kwamba hii ni klabu ya kihistoria yenye hadithi kubwa, na nikienda huko nahitaji kupigana, kwa klabu, kuwa tayari, kwa sababu hii ndiyo klabu kubwa zaidi duniani kwangu, ilikuwa vizuri kuzungumza kuhusu hili."

Mahojiano hayo yalichukua muda mfupi wakati Yoro akioneshwa video ya Ferdinand, wakati ambapo gwiji huyo wa klabu alishiriki ujumbe wa kumtia moyo nyota huyo mchanga.

Alisema: "Una uwezo wote, una zana zote, bwana, una kila kitu hapo, tayari kuyumba na kusonga mbele na kufanya athari kubwa kwenye kilabu hiki."

Yoro ambaye alishangazwa na ujumbe huo aliendelea: "Huo ni wazimu. Nilipokuwa mdogo, Rio alikuwa mmoja wa mabeki bora zaidi duniani.




# Højbjerg atua Marseille

**MARSEILLE,** Ufaransa

KLABU ya Marseille imekamilisha usajili wa kiungo mkabaji, Pierre-Emile Højbjerg, kutoka Tottenham Hotspur kwa mkopo wa awali na wajibu wa kumnunua.

Mkataba huo unaripotiwa kuwa na thamani ya Euro milioni 20, huku Højbjerg akimfuata Mason Greenwood wa Manchester United kujiunga na Marseille, inayonolewa na kocha wa zamani wa Brighton, Roberto De Zerbi.

Højbjerg mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Spurs kutoka Southampton mwaka 2020 na kucheza mechi 184 katika klabu hiyo ya Kaskazini mwa London, akifunga mabao 10.

Alishiriki katika mechi 36 za Ligi Kuu England kwa Spurs msimu uliopita, ingawa 26 kati ya hizo aliingia kama wa akiba.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark, alianza soka lake la kulipwa akiwa na Bayern Munich kule Bundesliga, akipata uzoefu wa mkopo kwenda Augsburg na Schalke.

Ameichezea nchi yake mechi 81, akifunga mabao 10, na alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshiriki michuano ya Euro 2024.

# De Bruyne hataondoka Man City – Guardiola

**NORTH CAROLINA,** Marekani

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema ripoti zinazomhusisha Kevin De Bruyne kuondoka katika klabu hiyo si sahihi huku kukiwa na uvumi kwamba kiungo huyo wa Ubelgiji huenda akahamia Saudi Arabia.

De Bruyne, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2025, alisema mwezi uliopita kwamba hakatai kuhama, lakini Guardiola anaamini hakutakuwa na mabadiliko makubwa kwenye kikosi kabla ya kumalizika kwa dirisha la uhamisho, ambalo litafungwa Agosti 30, mwaka huu.

"Kevin haendi," alisema Guardiola katika mkutano na waandishi wa habari katika Chuo Kikuu cha Jimbo la North Carolina Jumatatu kabla ya mechi yao ya ufunguzi ya ziara ya Marekani dhidi ya Celtic.

"Nimefurahishwa na kikosi kwa miaka mingi, sijui nini kitatokea sokoni, mtu akiondoka tutazungumza hilo.

"Lakini kwa asilimia 85 hadi 95 tutakuwa na kikosi sawa. Tumeleta matokeo sokoni zaidi ya miaka na kila hali ni tofauti. Najisikia raha kwa sababu ubora tulionao kwenye kikosi ni vigumu kuchukua nafasi."

City ilimsajili winga wa Brazil, Savio mwenye umri wa miaka 20, wiki iliyopita na Guardiola alithibitisha kwamba Kalvin Phillips, ambaye alikuwa kwa mkopo West Ham United, amekuwa akifanya mazoezi na kikosi cha kwanza.

"Savio anaweza kucheza kwenye winga," aliongeza Guardiola.

"Wachezaji wengi wanataka kuja hapa, lakini hatukupata makubaliano kutoka kwa klabu."

City wataanza kutetea taji lao la Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea Agosti 18, mwaka huu.



HABARI MICHEZO

## Balozi: Kwa Simba hii timu zijipange

INATOKA UK. 24

huu, mimi mwenyewe nina furaha, tulikuwa na wiki mbili ngumu ya kukiandaa kikosi, tulikuwa tunahitaji kucheza na kushinda, lakini tulihitaji pia wachezaji wetu wawe na muunganiko na mawasiliano baina yao wenyewe uwanjani.

"Baadhi ya wachezaji wamecheza dakika 60, wakati mwingine nilifanya mabadiliko kutokana na jinsi ninavyoona mchezo unavyokwenda, tulianza vizuri tukafunga mabao mawili haraka, tukapoteza nafasi nyingi hasa kipindi cha kwanza, bado hatuna uwezo wa kucheza dakika zote 90 kwa kasi ile ile, kwa sababu tuna wiki mbili tu, tunahitaji kiasi cha wiki nne au tano za mazoezi, tunahitaji muda," alisema.

## Gamondi: Dube bado, afadhali kidogo Baleke

INATOKA UK. 24

Mzambia, Clatous Chama dakika ya 90, na wote hao wamesajiliwa na Yanga kuelekea msimu ujao wa mashindano.

Baada ya hapo hakuonekana tena kutokana na kile kilichodaiwa kuwapo na mgogoro wa kimkataba baina yake na Klabu ya Azam ambao ulimalizika hivi karibuni akitakiwa kuilipa timu yake ya zamani kiasi cha Sh. milioni 500 ili awe huru na hilo lilifanyika kabla ya kutimkia Jangwani.

Kwa upande wa Baleke, baada ya kuachwa na Simba kipindi cha dirisha dogo Januari mwaka huu alitimkia Al Ittihad ya Libya na sasa ameonekana akiwa na kikosi cha Yanga na kufunga bao la kufutia machozi kwenye mechi ya Jumamosi dhidi ya Augsburg, ingawa hajatambulishwa rasmi.

Akizungumza mechi ya leo alisema atahakikisha kila mchezaji anapata fursa ya kuonyesha uwezo wake kwa sababu hakuna idadi maalum ya kuingiza wachezaji wa akiba.

"Nitampa nafasi kila mchezaji kucheza angalau kwa dakika 15 ili kuonyesha uwezo walionao na kuwafanya wawe na utimamu wa mwili, tunakwenda hivyo hivyo taratibu, kidogo kidogo lakini kwa uhakika," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Baada ya mechi hiyo, Yanga itakamilisha mechi zake Jumapili, ambapo inatarajiwa kucheza mchezo wa Kombe la Toyota, dhidi ya Kaizer Chief ya nchini humo itakayopigwa Uwanja wa Bloemfontein.

# KIBU KIKAANGONI, COASTAL IKILIA NA SIMBA KWA LAWI

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI uongozi wa Klabu ya Simba ukisema haujui alipo kiungo mshambuliaji wao, Denis Kibu na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake pindi atakaporejea, Klabu ya Coastal Union nayo imesema inawasubiri 'Wekundu wa Msimbazi' hao kukaa meza moja ili kulimaliza suala la beki Lameck Lawi.

**Simba tayari wametimiza wiki tatu katika kambi yao kwenye mji wa Ismailia nchini Misri, lakini Kibu ni mmoja wa wachezaji ambaye hajaripoti kambini mpaka sasa.**

Mchezaji mwingine ambaye hayupo kwenye kambi hiyo ni golikipa, Aishi Manula, ambaye bado yupo nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema uongozi wa klabu hiyo hauna taarifa ya wapi alipo Kibu na kwa sasa taratibu nyingine za ndani zinafanyika kumwadhibu mchezaji huyo.

"Hatujui wapi alipo, mara ya mwisho uongozi ulikuwa unafahamu amekwenda Kigoma mara moja baada ya kurudi kutoka mapumzikoni Marekani, lakini mpaka sasa hivi hatuna taarifa nyingine na hapatikani kwenye simu," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kuwa zipo taratibu za ndani, Simba kama taasisi ambazo watazichukua juu ya mchezaji huyo.

"Simba ni taasisi kubwa ina mifumo yake, hili suala litafika kwa uongozi na watachukua hatua stahiki kwa mchezaji husika, ni kosa kutokuwapo kwenye kambi ya timu bila sababu," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine, Ahmed alisema golikipa Manula muda wowote kuanzia sasa ataungana na wachezaji wenzake katika kambi nchini Misri.

"Manula bado ni mchezaji wa Simba, na nakuhakikishia muda wowote kuanzia sasa ataungana na wenzake kambini kuendelea na maandalizi," alisema Ahmed bila kutoa ufafanuzi zaidi.

Kuhusu Lawi, Klabu ya Coastal Union imesema inausubiri uongozi wa Simba wakae meza moja kulimaliza pembeni sakata la usajili wa beki huyo.

Ikumbukwe baada ya Simba kupeleka malalamiko yao kwa Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), juu ya sakata hilo la usajili, klabu hizo zilitakiwa kukaa meza moja na kumalizana juu ya usajili wa mchezaji huyo ambaye Simba wanadai wamemsajili kihalali huku Coastal Union wakikana kwa kile wanachodai wenzao hao hawakufuata makubaliano yao.

Msemaji wa Coastal Union, Abbas El Sabri, alisema jana kuwa wao wanawasubiri mezani Simba kama walivyoshauri kamati hiyo ya TFF.

"Ni kweli tulipewa ushauri huo, sisi hatuna shida tunawasubiri wenzetu wa Simba watakapokuwa tayari tukutane kulimaliza suala hili, kama tulivyosema awali sisi hatua shida, Simba wakiwa tayari tutaenda kukutana nao," alisema El Sabri.

Hata hivyo, El Sabri alikiri licha ya mchezaji huyo kumworodhesha kwenye usajili wao msimu ujao, kwa sasa yupo nje ya nchi kwa mambo yake binafsi.

"Lawi yupo Ubelgiji kwa mambo yake binafsi, lakini ni mchezaji wa Coastal na tumepeleka jina lake CAF kwa ajili ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo tutashiriki msimu ujao," alisema El Sabri.

Kwa upande wake, Msemaji wa Simba, Ahmed Ally, alisema kuwa suala hilo linashughulikiwa na uongozi wa juu wa klabu hiyo.

"Kama kutakuwa na lolote wana Simba watafahamu, kwa sasa suala hilo lipo ngazi ya juu na limefika TFF, mbivu na mbichi zitajulikana hapo pande zote zitakapokutana," alisema Ahmed.

KAZINI LEO...



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akifanya mazoezi gym nchini Afrika Kusini jana kuelekea mechi yao ya leo dhidi ya TS Galaxy kuwania Kombe la Mpumalanga. **PICHA: YANGA**

## *Azam: Hatutafuti ushindi Morocco*

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kucheza mchezo mmoja wa kirafiki nchini Morocco wakiwa kwenye kambi ya maandalizi kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema kwenye michezo hiyo hawaangalii matokeo bali kile wanachowafundisha wachezaji wao kama wamekishika.

Azam juzi ilicheza na Union Yacoub El Mansour inayoshiriki Ligi Daraja la Tatu nchini humo na kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dabo, alisema bado wanaendelea na maandalizi yao na kwa kiasi kikubwa wachezaji wake wanafuata kile wanachowaelekeza kwenye mazoezi yao.

Alisema kambi ya timu hiyo ni kwa ajili ya kuandaa timu kwa kuwapa mbinu mbalimbali pamoja na kutengeneza muunganiko mzuri kwenye kikosi, hivyo hawaangalii sana matokeo wanayoyapata.

"Tunataka kuona kile tunachowapa kwenye mazoezi wanakishika na kukifanyia kazi kwenye mechi, tunashukuru taratibu wachezaji wanachukua tunachowapa, tunaangalia namna wanavyocheza, hii kambi itatusaidia sana," alisema Dabo.

Alisema wanataka kucheza angalau mechi tatu kabla ya kurejea nchini kwa ajili ya mchezo wao wa Ngao ya Jamii dhidi ya Coastal Union utakaochezwa Agosti 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Mshindi kwenye mchezo huo atacheza na timu itakayoshinda kati ya Simba na Yanga ambao wenyewe utachezwa siku hiyo hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Michezo

Jumatano Julai 24, 2024

Nipashe



Kane kuikosa Spurs UKURASA 21




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Charles Ahoua, akifunga moja kati ya mabao mawili aliyofunga juzi wakati wakishinda 3-0, katika mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya El Qanah FC ya Misri iliyopigwa Uwanja wa Old Suez Canal, Misri. **PICHA: SIMBA**

## Gamondi: Dube bado, afadhali kidogo Baleke

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, Miguel Gamondi, amesema mchezaji wake Prince Dube hayupo kwenye kiwango bora, ikiwamo kutokuwa na utimamu kwa mwili kutokana na kutocheza soka kwa muda mrefu, huku akibainika angalau Jean Beleke alionyesha ana afadhali.

Akizungumza jana kuelekea katika mchezo wa leo wa Kombe la Mpumalanga dhidi ya TS Galaxy, utakaochezwa jioni kwenye Uwanja wa Mbombela nchini Afrika Kusini, Gamondi, alisema Dube hayupo kwenye kiwango chake ndiyo maana ubora wake haukuonekana katika mechi dhidi ya Augsburg ya Ujerumani, ambao walichapwa mabao 2-1.

"Nafikiri wachezaji walicheza vizuri mechi iliyopita, lakini baadhi hawakufanya vizuri kwa sababu hawajacheza muda mrefu, mfano Dube, hakuwa uwanjani kwa zaidi ya miezi sita, Baleke alikuwa na afadhali kidogo, lakini wengine wanaonekana wako fiti, ila bado baadhi wanatakiwa wazoeane na wenzao, kujua wenzake wanapasiwa vipi mpira, na yeye mwenyewe mchezaji



anatakiwa awe wapi ili apokee pasi kutoka kwa wenzake.

"Kiujumla kuna baadhi ya wachezaji wanatakiwa wazoeane na wenzao ili kujua wachezeje, ila kwa ujumla kila kitu kinakwenda sawa," alisema Gamondi.

Mara ya mwisho Dube kuonekana uwanjani akicheza mechi ya ushindani ilikuwa ni Februari 9, mwaka huu, wakati timu yake ya Azam ikicheza dhidi ya Simba katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1, Mzimbabwe huyo akipachika bao dakika 14, kabla ya kusawazishwa na

INAENDELEA UKURASA 23

# *Balozi: Kwa Simba hii timu zijipange*

**Na Adam Fungamwango**

●●● Asifu waliofanya usajili, Kocha Fadlu naye asema hapo bado anahitaji wiki nne hadi tano ili...

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, akionekana kufurahishwa na ushindi ambao timu yake iliupata juzi dhidi ya El Qanah, lakini akisema bado anahitaji muda ili wachezaji wake wafanye vile anavyotaka, Balozi wa Tanzania nchini Misri, Meja Jenerali Richard Mutayoba Makanzo, amekimwagia sifa kikosi hicho, akizitahadharisha timu za Ligi Kuu Tanzania Bara zijipange kukabiliana nayo.

Akizungumza baada ya mechi ya kirafiki na timu hiyo inayocheza Ligi Daraja la Pili, iliyochezwa Ismailia nchini Misri, Simba ikishinda mabao 3-0, Balozi huyo aliwasifia watu waliofanya usajili wa wachezaji hao, akisema kwa macho yake amekuwa mmoja kati ya Watanzania wa mwanzo kukiona kikosi hicho, chenye wachezaji wanaotandaza kandanda la uhakika.

**"Naipongeza timu iliyofanya usajili kwa kweli imesajili vijana wazuri sana, nimewaona mwenyewe kwa macho yangu, wanacheza mpira safi sana, na tuseme tu msimu unaoanza timu nyingine nyumbani zijipange, Simba wako vizuri sana," alisema Makanzo.**

Balozi huyo ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye mchezo huo uliopigwa juzi jioni katika Uwanja wa Old Suez Canal, alisema atakuwa na kikosi hicho kipindi chote ambacho watakuwa nchini humo, ikiwamo kurejea tena kuwapa nguvu katika mchezo mwingine utakaofuata.

"Mimi kama balozi, nawaahidi nitakuwa nanyi kwa kipindi chote mtakachokuwa hapa Misri na nitakuja tena ili kuwapa nguvu kwa mchezo utakaofuata, hongereni kwa ushindi mzuri, lakini kikubwa tulikuwa tunatazama jinsi mnavyocheza.

"Mngeamua kukaa Tanzania, lakini mmeamua kuja kukaa huku, tunajua ni gharama, lakini mmefanya heshima kwa nchi yetu kwa sababu mnaimarisha diplomasia ya mpira wa miguu na michezo kwa ujumla, hiki mlichokifanya mnatuongezea tuwe na mahusiano mazuri na nchi hii, hongereni sana," alisema.

Katika mechi hiyo, Simba ilishinda mabao 3-0, katika mchezo uliochezwa kwa dakika 120, kwa vipindi vitatu vilivyochezwa kwa dakika 40 kila kipindi.

Mabao ya Simba yalifungwa na wachezaji wapya ambao ni Jean Charles Ahoua, aliyesajiliwa kutoka Stella Club d'Adjame ya nchini Ivory Coast, dakika ya 14 na 16, na Augustine Okejepha namba sita ya 'boli' kutoka Rivers United ya Nigeria dakika ya 120.

Kocha Fadlu baada ya mechi hiyo alisema anajivunia ushindi wa vijana wake, lakini akisema anahitaji muda zaidi ili wawe fiti kwani wana wiki mbili tu, ambapo ili waweze kucheza anavyohitaji anahitaji wiki nne mpaka tano.

"Inapaswa tujivunie na ushindi

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >